# Nipashe

Jumanne Mei 5, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580223

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

n digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Wabunge 11 wa Chadema wakaidi maagizo ya Mbowe

UKURASA 2



Nipashe TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Utaratibu huu ungewezesha kupata mafao kwa wakati

Corona yachochea njaa Afrika Congo, Nigeria, Sudan kusota

ELIMU

NA SABATO KASIKA

Ndivyo jamii inavyojipanga kuongeza madarasa 2021

UKURASA 11

# Vigogo wa 'maabara ya corona' wasimamishwa

• **Ni** baada ya vipimo kuonyesha papai, mbuzi wako 'positive', kamati ya maprofesa yaundwa kuchunguza... *Endelea ukurasa 2*



**BAA LA CORONA**

**Ili kujikinga na virusi vya corona, hakikisha usafi wa mikono yako ni muhimu kila wakati na ni njia nzuri ya kuwakinga wengine. WHO**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya, kukohoa, ziba mdomo**

RIPOTI MAALUMU

## Hii ndiyo hali ya chakula nchini

UKURASA 4




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu. Dk. Nyambura Moremi




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## CCT yashauri serikali kutoa majibu wanaokufa corona

UKURASA 15


**MICHEZO** **LIGI KUU BARA KUREJEA JUNI** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

**HABARI KITAIFA**

# Vigogo 'maabara corona' wasimamishwa kazi

**Na Romana Mallya**

SIKU moja baada ya Rais John Magufuli kushangazwa na maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii kutoa majibu ya sampuli za mimea na wanyama, zikidaiwa kuwa na virusi vya corona, vigogo wawili wa maabara hiyo wamesimamishwa kazi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia kwa Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali Idara Kuu, Afya, Catherine Sungura, waliosimamishwa kazi ni Mkurugenzi wa Maabara hiyo, Dk. Nyambura Moremi, na Meneja Mdhibiti wa Ubora, Jacob Lusekelo.

Juzi, baada ya Rais Magufuli kumwapisha Waziri mpya wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, mjini Chato mkoani Geita, alibainisha dosari za utendaji wa maabara hiyo baada ya 'kuichomekea' sampuli za mimea na wanyama na majibu yake kurejeshwa yakionyesha baadhi zimeathirika kwa virusi vya corona.

Kutokana na agizo la Rais kuchunguzwa kwa utendaji wa maabara hiyo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amelazimika kuchukua hatua kwa kumwelekeza Katibu Mkuu wake kuwasimamisha kazi mara moja viongozi hao wawili ili kupisha uchunguzi.

"Waziri ameunda kamati ya wataalamu wabobezi kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa mwenendo wa maabara hii ikiwamo mfumo mzima wa ukusanyaji na upimaji wa sampuli za corona," ilibainishwa katika taarifa ya wizara hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kamati hiyo ya uchunguzi itaongozwa na Prof. Eligius Lyamuya kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (Muhas) na itakuwa na wajumbe tisa.

"Wajumbe hao ni Prof. Said Aboud (Muhas), Prof. Gabriel Shirima (Chuo Kikuu cha Nelson Mandela - NMIST), Prof. Steven Mshana (Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Bugando - Cuwas) na Prof. Rudovick Kazwala (Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine - SUA).

"Dk. Thomas Marandu (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - UDSM), Dk. Mabula Kasubi (Hospitali ya Taifa ya Muhimbili - MNH), Dk. Danstan Hipolite (Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba - TMDA), Viola Msangi na Jaffer Sufi (wataalamu wa maabara wastaafu)," ilibainisha.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya wizara, kamati hiyo inatakiwa kuanza kazi mara moja na itatakiwa kuwasilisha taarifa yake kwa Waziri Ummy kabla ya Mei 13 mwaka huu.

"Sambamba na uchunguzi wa kamati hii, shughuli za upimaji wa sampuli katika maabara hii zinaendelea," ilibainisha.

Katika hotuba yake, Rais Magufuli alisema uamuzi wa kuwasilisha katika maabara hiyo sampuli za mimea, wanyama na kemikali, ulitokana na uchunguzi wa siri wa serikali dhidi ya utendaji wa chombo hicho, baada ya kukitilia shaka.



Mshtakiwa raia wa Burundi, mkazi wa Kijiji cha Rungwe Mpya, Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma , Yohana Filipo, akiwa chini ya ulinzi wa askari Polisi baada ya kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa katika Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma jana, kwa kosa la kumuua mkewe. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Wabunge 11 wa Chadema wakaidi maagizo ya Mbowe

**Na Salome Kitomari**

WABUNGE 11 wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), jana walikaidi maagizo ya Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, kuwataka kutohudhuria vikao vya Bunge na kujitenga kwa siku 14.

Wabunge hao na majimbo yao kwenye mabano ni Joseph Selasini (Rombo), Peter Lijualikali (Kilombero), David Silinde (Momba), Antony Komu (Moshi Vijijini), Susan Masele (Viti Maalum), Jaffary Michael (Moshi Mjini) na wa Viti Maalum; Latifa Chande na Subrina Sungura, Cecilia Pareso, Joyce Sokombi na Mariam Msabaha.

Wabunge hao walihudhuria mkutano wa 18 wa kikao cha 21 cha Bunge la 11 jana, kilichojadili na kupitisha makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na walikuwa katika ukumbi wa Msekwa na ukumbi mkuu wa Bunge.

Mbunge Selasini wiki iliyopita alilalamika bungeni kwa kuondolewa kwenye kundi songezi la wabunge wa Chadema na kushindwa kuchangia mjadala wowote tangu kuanza kwa Bunge, hadi alipopitia kwa Spika, Job Ndugai.

Aidha, siku iliyofuata Selasini alitangaza kuendelea kuwa mbunge, lakini hana mpango wa kugombea kupitia Chadema, bali NCCR- Mageuzi, Oktoba mwaka huu.

Februari mwaka huu, Komu alitangaza kuwa atagombea ubunge jimbo hilo, na kwamba wakati ukifika atagombea kupitia NCCR- Mageuzi.

Silinde alikuwa wa pili kuchangia mjadala wa wizara hiyo, pamoja na mambo mengine, alisema wajibu wa Bunge ni kupambana hadi mwisho na si vinginevyo.

"Corona ni janga la kimataifa linalohitaji nguvu ya pamoja, siyo janga la mtu mmoja ama chama fulani cha siasa, dunia inalia na sisi Watanzania hatupaswi kulia... tunapaswa kuchukua hatua kupambana ili kuwasaidia wananchi wetu walioko nje (Bunge). Na huo ndiyo wajibu wa kibunge, ni kupambana mpaka dakika ya mwisho," alisema.

Akizungumza na Nipashe, Mbunge wa Moshi Mjini, Michael, alisema: "Nipo ukumbini Msekwa. Kuwapo kwangu siyo kutokutii maagizo ya Mbowe kwa kuwa Mwenyekiti wetu kama kiongozi wetu ana wajibu wa kulinda afya na maisha ya wabunge wake.

Akichangia, Selasini alisema: "Huu ni mkutano wa mwisho wa bunge la 11, kama kuna haja liahirishwe kabla ya muda wake wa kisheria upo utaratibu, tunaweza kumuomba Rais kwa kutumia kanuni ya 30 ya Bunge na siyo kutoka kabla ya wakati bila utaratibu kufanyika," alisema.

Mwishoni mwa wiki, Mbowe aliwataka wabunge hao kujitenda na wasisafiri kwenda majimboni au mikoani hadi baada ya siku 14 kwisha, kwa ajili ya kujikinga na maambukizo ya corona.

Aidha, wabunge hao walitakiwa kutofika kabisa eneo la Bunge Dodoma na Dar es Salaam.

Mbowe walilitaka bunge kuhairisha shughuli zake kutokana na tishio la corona, na baadhi ya vikao kufanyika kwa njia ya mtandao, na kuwashauri wabunge wengine kutohudhuria.

Tangu kuanza kwa bunge hili la mwisho wabunge watatu wamefariki ambao ni Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mch. Dk. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Sumve, Richard Ndassa na Waziri wa Katiba na Sheria ambaye ni Mbunge wa kuteuliwa, Balozi Dk. Augustino Mahiga.

# Ahukumiwa kunyongwa kumuua mke makusudi

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Kigoma imemhukumu raia wa Burundi, mkazi wa Kijiji cha Rungwe Mpya, Wilaya ya Kasulu, Yohana Filipo (28) kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumuua kwa makusudi mke wake wa zamani Scolastica James kwa kumchoma kisu shingoni na kufariki dunia.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji wa Mahakama hiyo, Athumani Matuma, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo.

Alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa vijana wengine wenye tabia ya kikatili kama yake.

Alisema upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi watano na vielelezo viwili ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kwa makusudi.

Jaji Matuma alisema mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Oktoba 23, 2017 majira ya jioni katika Kijiji cha Rungwe mpya eneo la mashambani, Wilaya ya Kasulu, mkoani Kigoma.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Robert Magige, ulipeleka mahakamani mashahidi watano na upande wa utetezi mshtakiwa alijetetea mwenyewe kwa kuongozwa na wakili wa kujitegemea Diana Damson.

Alisema wakati wako mashambani Scolastica James na Shamini Moshi, walienda mtoni kuchota maji wakati wakiwa wamebeba ndoo zao kichwani, ghafla mshtakiwa alimvamia Scolastica na kumchoma kisu shingoni na kukosa hewa baada ya kuvuja damu nyingi na alifariki dunia.

Jaji Matuma alisema shahidi wa kwanza upande wa mashtaka Shamini Moshi, alieleza mahakamani kuwa yeye na merehemu walikuwa wanatembea wakiwa wamebeba ndoo zao kichwani na mshtakiwa alimpita na kwenda mbele yake na kumchoma kisu Scolastica majira ya saa 12 jioni yeye akiwa umbali wa mita nne na alishuhudia kwa macho yake mshtakiwa akimchoma kisu Scolastica.

"Mimi jaji naungana na wazee wawili washauri kuwa kitendo alichokifanya mshtakiwa huyu ni kitendo cha makusudi, pia alipanga kufanya ukatili huu."

## HABARI KITAIFA

# Takukuru yaokoa mil. 57/- vyama ushirika

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Morogoro imeokoa Sh. milioni 57.8 zilizokuwa mikononi mwa viongozi wa vyama vya ushirika na Saccos katika wilaya za Mvomero na Gairo.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari, Naibu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Morogoro, Victor Swella, alisema bado watuhumiwa wengine waliochota fedha hizo wanaendelea kurejesha ambazo walizifanyia ubadhirifu kinyume na malengo ya vyama hivyo.

"Tumeokoa Sh. 57,879,725 ambazo zilikuwa mikononi kwa viongozi wa vyama vya ushirika na Saccos kwenye wilaya ya Mvomero na Gairo," alisema Swella.

Alisema katika kipindi hicho, Takukuru ilibaini kuwapo kwa wateja sugu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro kutolipa madeni yao yaliyotokana na huduma ya majitaka.

Naibu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Morogoro, alisema katika ufuatiliaji huo Mamlaka hiyo imeendelea kulipwa fedha toka kwa wateja hao.

Alisema katika kukabiliana na ubadhirifu huo, mamlaka hiyo imelipwa Sh. 4,238,107.80 kati ya Sh. 13,386,932.40 zinazodaiwa kwa wateja waliotumia huduma hiyo.

Akizungumzia ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo, alisema Takukuru ilibaini kuwapo kwa ukiukwaji wa masharti ya vipengele vya mkataba ulioingiwa kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi pamoja na Kampuni ya ujenzi ya Deep Construction Ltd kwa gharama ya Sh. 225,061,990.

Swella, alisema gharama hizo ni kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi na pia Sh. 123,273,499.90 kwa ajili ya ujenzi wa dampo.

Hata hivyo, alisema Takukuru imeweka mikakati au maeneo ya kipaumbele kwa kipindi cha Aprili hadi Juni, mwaka huu kufuatilia vitendo vyote vya rushwa kuekelea Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na madiwani, Oktoba mwaka huu.

"Tunaendelea na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo kwa kuwa fedha nyingi zinaelekezwa katika sekta ya maji, elimu na ujenzi wa miundombinu," alisisitiza.



Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kikrito Tanzania (CCT), Mchungaji Canon Moses Matonya, akizungumza na waandishi wa habari, ofsini kwake, jijini Dodoma jana, juu ya patano la viongozi wakuu wa makanisa wanachama wa jumuiya hiyo, kuhusu nafasi yao katika kupambana na ugonjwa wa corona. Habari Uk. 15. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Mazungumzo vigogo Halotel, DPP yafikia hatua za mwisho

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili vigogo sita wa Kampuni ya Viettel Tanzania akiwamo Mkurugenzi wa Kampuni ya Halotel, Son Nguyen (46), umedai kuwa mazungumzo ya kukiri makosa kati ya washtakiwa hao na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP) yamefikia hatua za mwisho.

Kadhalika Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai wanasubiri kibali kwa DPP ambaye yuko jijini Dodoma atakaporejea wataendelea kufuatilia.

Madai hayo yalitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, wakati kesi hiyo ya uhujumu uchumi kuisababishia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), hasara na kutakatisha zaidi ya Sh. bilioni 75 ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa.

Wankyo alidai kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa.

Wakili wa utetezi Majura Magafu, alidai washtakiwa waliandika barua kwa DPP ya kutaka kukiri makosa yao mapema Aprili 21, mwaka huu.

Wankyo alijibu kwamba barua ya washtakiwa imepokelewa, tayari na majadiliano yameanza na wamekamilisha kwa kiasi kikubwa, kinachosubiriwa ni hati ya DPP ya kuipa mamlaka Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kuendelea na kesi hiyo.

"Mheshimiwa hakimu DPP yuko Dodoma hivyo akirudi tutaendelea kufuatilia, tunaiomba mahakama ipange kesi hii baada ya siku 14 au wakikamilisha kabla ya siku hizo washtakiwa watapelekwa mahakamani," alidai Wankyo.

Hakimu alisema mahakama yake imekubali ombi la Jamhuri, kesi hiyo itatajwa Mei 18, mwaka huu.

Awali, mahakamani hapo upande wa Jamhuri ukiongozwa na Monica Mnogo, uliwataja washtakiwa wengine kuwa ni, Nguyen Minh (40) na Vu Tiep, wote mameneja wa Halotel, Ha Than (39), mtaalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) Halotel, Mkurugenzi wa fedha wa kampuni hiyo, Nguyen Cong na Kampuni ya Viattel.

Mbogo alidai kuwa kati ya Juni 8, 2017 na Machi 26, 2020 eneo la Mikocheni, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao waliongoza genge la uhalifu ili kujipatia faida.

Alidai kuwa kati ya Juni 8, 2017 na Machi 26, mwaka huu eneo la Mikocheni Wilaya Kinondoni, jijini Dar es Salaam na maeneo mengine ya nchi kwa pamoja walitumia masafa ya redio bila kupata kibali kutoka TCRA.

Pia alidai kati ya Julai 7, 2016 na Machi 26, mwaka huu kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Vietnam kwa pamoja walitengeneza mfumo ambao ulitumia huduma za mawasiliano zinazojulikana kama Virtual Private Network (VPN), kinyume cha taratibu.

Katika shtaka la nne, inadaiwa washtakiwa hao walikwepa kulipa kodi kwa TCRA kwa kutumia mitambo ya mawasiliano iliyounganisha Viettel Tanzania na Vietnam kinyume na sheria.

Ilidaiwa Juni 8, 2017 na Machi 26, mwaka huu eneo la shtaka la nne kwa kutumia masafa ya redio bila kupata kibali cha TCRA walisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 75.

# Bandari kavu Pwani kukamilika Julai

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Deusidedit Kakoko, amesema utekelezaji wa mradi wa Bandari Kavu ya Kwala iliyopo Kibaha mkoani Pwani, unatarajiwa kukamilika Julai mwaka huu.

Kakoko alisema mradi huo utatekelezwa katika hekta 60 kati ya 500 za eneo lililotwaliwa na mamlaka hiyo katika Kata ya Kwala chini ya Mkandarasi Suma JKT kwa gharama ya Sh. bilioni 47.

Alisema awamu ya kwanza ya mradi huo ilihusisha ufyekaji wa eneo la hekta 120, usawazishaji, kujaza kifusi, matabaka ya changarawe na ujenzi wa reli wa kilomita 1.3 kutoka kituo cha Kwala hadi bandarini hapo.

Awamu ya pili, alisema ilihusisha kunyanyua tuta, kumwaga zege na kuweka reli tano zenye urefu wa mita 500 na kuzungusha ukuta wenye urefu wa kilomita 3.2.

Kakoko alisema awamu hiyo pia inahusisha uwekaji wa miundombinu ya huduma za umeme, maji, mawasiliano na vizima moto pamoja na ujenzi wa nyumba za muda za watumishi na ofisi.

Alisema hadi sasa mkandarasi ameshalipwa Sh. bilioni 20.5 sawa na asilimia 45 huku mradi ukiwa asilimia 70.

Alisema awamu ya tatu inayofuata ni ujenzi wa barabara ya kilomita 15.5 kwa kiwango cha changarawe ikiwa ni hatua za awali za kuijenga kwa kiwango cha zege na kwamba barabara hiyo itaunganisha bandari kavu ya Kwala na Barabara ya Morogoro eneo la Vigwaza.

Pia, bandari hiyo itaunganishwa na reli ya kisasa ya SGR ambayo itatumika kupeleka kontena mikoani na nje ya nchi.


## ANATAFUTWA



215728902

**GODLISTEN GODMERCY MBISE**

Mtajwa hapo juu anatafutwa na Polisi kwa tuhuma za kumuibia Mwajiri wake **RB. Namba HIM/RB/1668/2020.**

Kwa yeyote atakaye muona au mwenye taarifa za mahali alipo atoe taarifa kituo cha Polisi Himo, Kilimanjaro au kituo chochote cha Polisi kilicho karibu au apige simu namba **+255 272754422/7.**

# Waziri: Hii ndiyo hali ya chakula nchini

## Pamba, aendeleza alipoachia Majaliwa



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga

**Na Sanula Athanas,** ALIYEKUWA DODOMA

BAADA ya jana kupata ufafanuzi wa Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, kuhusu kishindo cha corona kwenye mazao makuu manne ya biashara nchini, mjadala wa Nipashe na waziri huyo leo unaangalia mustakabali wa akiba ya chakula nchini ilikosimama katika zama hizi za corona, pia harakati za kuliinua zao kongwe la pamba nchini. Endelea:

**SWALI: Hali ya chakula ikoje kwa sasa nchini na kwenye Ghala la Taifa? NFRA watanunua tani ngapi mwaka huu?**

**HASUNGA:** Bado tuko kwenye mchakato wa kuangalia kiasi gani watanunua, lakini kwa upande wa chakula, kwanza kama nchi, sisi mfumo wetu uko tofauti kidogo na nchi nyingi.

Chakula kingi mwananchi ananunua mwenyewe. Chakula ambacho kinahifadhiwa na Hifadhi ya Taifa ni chakula ambacho ni cha dharura. Hicho ndicho tunatunza. Mpaka sasa tuna tani 47,000 kwenye ghala.

Na nimezunguka nchi nzima, chakula ni kingi. Mwaka huu watu wamehamasika sana, wamezalisha sana, chakula ni kingi na sasa hivi mavuno yameanza. Maeneo mengi zaidi mahindi yameanza kukauka, mpunga uko tayari unavunwa na vyakula vingine vingi.

Kwa hiyo, sasa chakula ni kingi na nina imani hali ikiendelea kama hivi, Watanzania kwa upande wa chakula hatutakuwa na upungufu. Lakini sasa kama NFRA tunataka tufanyeje?

Kwanza, tumeimarisha uwezo wetu wa kuhifadhi. Uwezo wetu ulikuwa ni kuhifadhi tani 251,000. Baada ya kuanza kujenga haya maghala ya kisasa, tunaongeza uwezo wa kuhifadhi kwa tani 250,000.

Ina maana kwamba NFRA itakuwa na uwezo wa kununua na kuhifadhi kwa wakati mmoja tani 501,000. Ina maana uwezo umeongezeka mara mbili.

Na tayari tumeagiza NFRA wanunue mazao hayo kwa njia mbili; ya kwanza watanunua yale ambayo ni kwa ajili ya kutunza kwenye Hifadhi ya Taifa. Tutawapa fedha ambayo tutaitenga kwenye bajeti pamoja na hiyo akiba ambayo wanayo. Tutahakikisha tunahifadhi kwenye Hifadhi Taifa tani zisizopungua 120,000. Huo ndiyo utaratibu tunaoutaka.

Halafu tunataka sasa karibu tani 400,000 wawe na uwezo wa kununua na kuuza, waingie kwenye mikataba ya kununua na kuuza. Kwa mfano, WFP wanahitaji, watanunua, yaani hata shirika lolote litakalokuwa linahitaji, nchi za nje watakapokuwa wanahitaji, wanunue kutoka NFRA.

Tunataka wafanye hivyo na ndiyo maana tumewapa mamlaka sasa waweze kukopa hela kama hawana fedha za kutosha au wawe na mikataba mizuri na wale wanunuzi, wawanunulie kusudi hilo lifanyike.

Kwa hiyo, tuna imani tutakuwa tumetengeneza soko kwa wakulima, lakini pia tutakuwa tumewezesha shirika letu uwezo wa kufanya kazi kwa mwaka mzima.

**SWALI: Vita inayoongozwa na Waziri Mkuu kuibua tena zao la pamba, unaielezeaje ilikofika?**

**HASUNGA:** Kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais John Magufuli kwa jitihada walizokuwa wamezifanya, kwa sababu wakati mimi ninaingia, nilikuta tayari wameshaanza kuzifanya hizo jitihada za kufufua hili zao la pamba.

Kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na wadau wengine, tumehamasisha sana uzalishaji uongezeke na ndiyo maana utaona kwa mwaka huu tumepata tani 348,850 za pamba, lakini tunataka uzalishaji huu uongezeke.

Kufanikisha hilo, tumeamua kutafuta maeneo yanayofaa kwa uzalishaji wa mbegu za pamba. Pia, tunataka kuhamasisha wakulima waongeze tija badala ya kulima wanapata labda wastani wa kilo 200 kwa ekari, tunataka wapate kilo 1,000 mpaka 1,500 (ongezeko la kati ya asilimia 500 na 750).

Kwa hiyo, tunataka waongeze tija, waongeze matumizi sahihi ya viuatilifu, lakini mbolea zinazohitajika kwenye pamba, wengi wao watumie mbolea. Tunataka tuwe na mbolea ambazo wanaweza kuzitumia, lakini wanaweza kupanda kwa kilimo kile cha mstari, kitaalamu kabisa cha kamba iliyonyooka, kilimo kinapendekeza.

Kama yote hayo wakizingatia, tuna imani kwamba wanaweza kuongeza uzalishaji zaidi. Lengo letu sisi ni kufikia tani 600,000 kwa mwaka na hivyo kama tukifikia hicho kiwango, kiasi fulani, angalau hata nusu ya pamba hiyo iwe inatumika kwenye viwanda vya ndani na ile nyingine tuwe tunauza kama malighafi katika maeneo mbalimbali. Hilo ni jambo la kwanza.

La pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu amesimama kidete kuhakikisha viwanda vyote vile vya pamba, vile vilivyokuwa vinachambua pamba vinafufuliwa. Na sasa tumefikia viwanda vingi sana vilivyokuwa chini ya ushirika, tumeagiza vyote vifufuliwe, na vya watu binafsi navyo tunataka vifufuliwe.

Zaidi ya hapo, tunataka tuongeze zaidi viwanda vya kutengeneza nyuzi na tukitoka hapo, tunakwenda kwenye viwanda vya kutengeneza majola ili badala ya soko la pamba kutegemea twende kuuza nje ikiwa ni malighafi, tutengeneze nguo hapahapa nchini, watu wetu wapate nguo hapahapa zinazotokana na pamba yetu, na sisi wenyewe tuvae nguo za kwetu.

Hiyo tunaamini kwamba tutakuwa tumetengeneza ajira nyingi sana kwa Watanzania, lakini pia tutakuwa tumeongeza thamani na uchumi wetu utakuwa umekua vizuri sana kuliko kwenda kuuza nje ya nchi.

Pia, tumeamua Bodi ya Pamba kuiongezea uwezo, tumewapa mamlaka waajiri maofisa ugani wa kwao kwa ajili ya kusaidia utaalamu. Hii nayo ni sehemu ya jitihada ambazo tumeamua kuzifanya na tunafikiri itachangia sana kuongeza uzalishaji.

- **KESHO USIKOSE VYA SANDUKUNI, WAZIRI ANAPOTAJA VIZINGITI VINAVYOKWAZA KILIMO KUINUKA.**

HABARI KITAIFA

# Wenye ulemavu wataka marejesho mikopo kusitishwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SHIRIKISHO la Vyama Vya watu wenye Ulemavu (Shivyawata) wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, wameomba Halmashauri kusimamisha kwa muda marejesho ya mikopo waliyochukua hadi pale hali itakaporejea kuwa kawaida kutokana na biashara wanazofanya kusimamia.

Akizungumza na Nipashe Katibu wa Shivyawata, Happiness Matagi, alisema kutokana na ugonjwa wa corona, mambo mengi yamebadilika ikiwamo la hali ya kiuchumi kwa kundi hilo.

Happiness alisema, ni vema Halmashauri ikasitisha suala la mikopo kwa sasa kwani biashara walizokuwa wanafanya zimekuwa ngumu hazifanyiki kama ilivyokuwa kabla ya ugonjwa huo.

"Ombi letu kwa Halmashauri isitishe kudai mikopo waliyochukua watu wenye ulemavu, biashara zimekuwa ngumu hata fedha kwa ajili ya chakula imekuwa ngumu, hali ambayo inasababisha waliokopa kushindwa kurejesha kwa Aidha, aliwaomba wafadhili kujitokeza kuwasaidia vifaa kinga vya corona kwani wanashindwa kumudu gharama za manunuzi, hivyo kuwa katika hatari ya kupata maambukizo.

"Hatuwezi kununua barakoa, sabuni wala ndoo za maji, tunaona wafadhili wakitoa vifaa hivyo kwenye maeneo mengine... wafike na kituoni kwetu watusaidie tuweze kujikinga." alisisitiza.

Aidha, aliiomba jamii kutowanyanyapaa watu wenye ulemavu wa kuona na badala yake wawasaidie kwa kuwashika mikono wanapopita barabarani na mitaani, kwani kwa sasa kutokana na ugonjwa wa corona, wananchi wengi wanasita kuwasaidia, hivyo wengine kukumbwa na adha ya kutumbukia kwenye mitaro .

# Tiba asili wanaodai kutibu corona wapigwa marufuku

**Na Jumbe Ismailly,** IKUNGI

CHAMA cha Watafiti wa Malaria Sugu na Mazingira wa Tiba za Asili (Chawamamu) kimepiga marufuku waganga wa tiba asili wanaodai kutibu ugonjwa wa Covid-19 kutojihusisha na shughuli hizo.

Chama hiki kimesema kama wataendelea kujihusisha na kutoa dawa za tiba ya ugonjwa huo, kuna uwezekano wa kuwapotezea maisha wagonjwa wanaowahudumia.

Mkurugenzi wa Chawamamu Taifa, Mika Tano Likapakapa, alisisitiza alisema baada ya mlipuko wa corona, kuna watu waliojitokeza wakitembea mitaani wakiuza majani, huku wengine wakitembeza mizizi na kusingizia kwamba ni dawa za kutibu corona.

Mkurugenzi huyo alisisitiza kwamba siyo wataalamu wote wanaotoa tiba za asili wana uwezo wa kutibu corona, hivyo kutumia fursa hiyo kuiomba serikali kusimamia kwa karibu waganga wanaowadanganya wananchi kuwa wana uwezo wa kutibu ugonjwa huo na kuwachukulia hatua za kisheria mara moja.

"Nitoe rai kwa serikali yetu kwamba siyo wataalamu wote wana uwezo wa kutibu corona, hivyo isimamie hilo...vyombo vya dola visimamia hilo kwani linapotokea jambo wapo watu wasio waadilifu na wapo wasio waaminifu kwa kuwa linapotokea jambo wanajua ndiyo sehemu ya kupatia riziki," alibainisha.

Kwa mujibu wa Likapakapa waganga hao hawanabudi kutekeleza agizo hilo la chama hicho kwani suala hilo linahusisha uhai wa watu, na kuwa uhai wa watu huwa haujaribiwi.



Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Suleiman Mzee (wa tatu kushoto), akizungumza na maofisa kutoka Vyuo vya Mafunzo Zanzibar waliotembelea Makao Makuu ya Jeshi hilo, jijini Dodoma jana. **PICHA: MAGEREZA** .

# Manispaa yavunja mkataba kampuni ya ujenzi stendi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro, imeamua kuvunja mkataba na Kampuni ya Fast iliyopewa ujenzi wa stendi ya Kaloleni ya daladala na kuunda tume ya wataalamu itakayochunguza gharama zilizotumika na kampuni hiyo ili iweze kuwafungulia mashitaka ya madeni yaliyobakia.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Sheilla Lukuba, alisema hayo katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika mjini hapa.

Katika kikao hicho ambacho pia kilihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, ambaye alitaka kujua ukamilishaji wa stendi hiyo baada ya kusimama kwa muda mrefu na kusababisha daladala kushindwa kuegeshwa na maduka yaliyopo pembezoni mwa stendi hiyo kufungwa.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, alisema kwa sasa yapo matumaini ya kuendelea na ujenzi wa stendi ya daladala ya Kaloleni kufuatia kupata mkandarasi mpya kutoka kampuni ya ujenzi ya Nandhra ambayo ndiyo inayoendelea na ujenzi wa soko kuu la kisasa na stendi mpya ya daladala ya Mafiga.

Alisema kwa sasa mkandarasi yupo eneo la ujenzi na tayari ameshaanza kazi na amepewa muda wa miezi miwili ili kukamilisha ujenzi wa stendi hiyo.

Alisema ujenzi huo utagharimu Sh. milioni 640 ambazo ni mkopo wa Benki ya Dunia (WB) chini ya fedha za uboreshaji miji ( Urban Local Government Strengthening Program).

Alisema kufuatia kuvunja mkataba na Kampuni ya Fast iliyopewa kandarasi ya ujenzi wa stendi ya Kaloleni, tayari halmashauri imeunda tume ya wataalamu itakayochunguza gharama zilizotumika na kampuni ili waweze kuwafungulia mashitaka ya madeni yaliyobakia.

Lukuba, alisema Kampuni ya Fast ilichukua mkataba wa muda wa miezi mitatu na walipewa malipo ya awali Sh. milioni 108, lakini walishindwa kutekeleza mradi huo kwa wakati.

Lukuba alisema, licha ya kampuni hiyo kuongezewa muda wa siku 45 na Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, ilishindwa kukamilisha na kuukacha mradi huo.

Katika hatua nyingine Mkurugenzi huyo ameishukuru serikali kwa kuipatia halmashauri fedha za ujenzi wa mradi wa soko kuu la kisasa bilioni 17 na fedha ya stendi ya Mafiga ya daladala Sh. bilioni 5.2.

Pia, fedha za ukarabati Mto Kikundi kiasi cha Sh.milioni 774, Shule ya Sekondari Mji Mpya, Sh. bilioni 1.4 pamoja na ukarabati wa shule kongwe ya Sekondari Morogoro.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Chonjo aliwashauri madiwani wa baraza hilo kufuatilia kwa karibu ukamilishaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo ukiwamo wa stendi mbili za daladala ya Kaloleni na Mafiga pamoja na ujenzi wa soko kuu la kisasa la Morogoro liweze kufunguliwa ili wafanyabiashara wapate fursa ya kulitumia na manispaa kupata mapato yake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Walimu wamepewa haki wanayostahili

RAIS John Magufuli amesema licha ya shule kufungwa kwa muda usiojulikana kutokana na tishio la virusi vya corona, serikali itaendelea kuwalipa mishahara walimu na wafanyakazi wengine.

Alitoa kauli hiyo juzi wilayani Chato mkoani Geita, alipomwapisha Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba.

Machi 17 mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitangaza kufungwa kwa shule na vyuo kwa muda usiojulikana ili kudhibiti kusambaa kwa maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu.

Akitangaza uamuzi huo, Rais Magufuli alisema amepata uzoefu katika miezi kadhaa iliyopita ya ugonjwa huu, kuwa nchi ina waajiriwa wengi kama walimu, asilimia karibu 49 ya waajiriwa wote ni walimu.

Hata hivyo, alisema serikali imeendelea kulipa mishahara bila hata wao kufundisha, wakati nchi nyingi zimeshindwa kuwalipa.

Alisema anawathibitishia walimu kuwa serikali utaendelea kuwalipa mishahara yao mpaka shule zitakapofunguliwa, na wafanyakazi wengine serikali itaendelea kuwalipa mishahara mpaka mambo mengine yakae sawa, na kwamba hiyo ndiyo maana halisi ya kutoumiza uchumi kwa sababu janga la corona litaondoka.

Kauli ya Rais bila shaka itawarejeshea walimu matumaini, kwa kuwa wengi wao walishaanza kuwa na hofu na wasiwasi kuhusiana na hatima yao baada ya kufungwa kwa shule ikiwa moja ya tahadhari za kudhibiti maambukizo ya virusi vya corona nchini.

Walimu walikuwa wanapata hofu na wasiwasi kuhusu hatima yao kutokana na baadhi ya watu kutoa taarifa za uvumi kuwa itakuwa vigumu kwa serikali kuwalipa walimu mshahara kwa kuwa hawafundishi tangu shule zilipofungwa.

Vile vile, walimu walikuwa wanapata hofu kutokana na hali iliyoko katika mataifa mengine, ambapo baadhi ya wafanyakazi wa sekta binafsi pamoja na watumishi wa umeme kumekuwapo na changamoto ya kuwalipa mishahara.

Kadhalika, hapa nchini walimu katika baadhi ya shule binafsi wamekumbana na changamoto ya kulipa mshahara, baada ya wamiliki wa shule kudai kuwa hawana fedha za kuwalipa kutokana na shule kuendelea kufungwa.

Tunaona kuwa Rais magufuli ameondoa hofu hiyo, ambayo ingeweza kuwazidishia walimu hofu na wasiwasi, hivyo kuwakosesha morali wa kuendelea kuwafundisha watoto.

Tunaamini kuwa Rais aliamua kuvunja ukimya huo, baada ya kuzisikia taarifa mbalimbali za uvumi, ambazo siku hizi zinasambazwa kwa kasi kubwa kupitia mitandao ya kijamii.

Kwa hatua hiyo ya serikali pamoja na kuwahakikishia watumishi wengine wa umma uhakika wa kulipwa mishahara licha ya changamoto za corona, ni mzuri kwa kuwa utawafanya watumishi kujiamini na kuendelea kuchapa kazi, pamoja na kutoa huduma kwa tija na ufanisi.

Wakati serikali ikieleza msimamo wake kwa watumishi wake, hali siyo nzuri katika sekta binafsi, kutokana na kuathiriwa zaidi na janga la corona. Hali hiyo imesababisha hata mishahara kuwa changamoto kupatikana, hivyo kutishia ajira za wengi.


Tunaishauri serikali kuketi na uongozi wa sekta binafsi kuona athari zilizotokana na uginjwa huo kwa Tanzania pamoja na hatua zipi zichukuliwe kukabiliana nazo.

Kwa mfano, kama walimu katika shule binafsi wanakosa mishahara na kupoteza ajira, bila shaka sekta nzima ya elimu nchini itapata mtikisiko, kwa sababu watoto wengi wanasoma katika shule za binafsi.

Kutokana na hali hii, tunasisitiza kuwa kuna haja ya serikali na wadau kukutana na kushauriana namna ya kusaidiana kukabiliana na changamoto hizo ili taifa letu lisonge mbele.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Vipindi vya runinga, redio visipite watoto



Na Sabato Kasika

**WAKATI** huu ambao kuna tishio la maambukizo ya virusi vya corona, shule nazo zimebuni mbinu mbalimbali za kuhakikisha wanafunzi wao wanaendelea na masomo kama kawaida wakiwa nyumbani.

Hii inatokana na kwamba tangu katikati ya mwezi Machi mwaka huu, serikali ilifunga shule zote nchini na hata ufundishaji wa masomo ya ziada (tuition), kama njia mojawapo ya kuzuia kuenea kwa maambukizo ya virusi vya corona.

Kwa sasa baadhi ya shule zinawatumia wanafunzi masomo kwa njia ya mtandao au wazazi na walezi kila mmoja kwa nyakati tofauti kwenda shuleni kufuata masomo hayo kwa ajili ya mtoto wake.

Lakini, pia kuna vipindi vya masomo kwa njia ya televisheni na redio ambavyo serikali imevianzisha lengo likiwa ni kuhakikisha wanafunzi wanasoma wakiwa kwenye likizo hiyo.

Hizi zote ni njia mojawapo ambazo zinaweza kusaidia kuepusha mkusanyiko shuleni au kuwakusanya wazazi na kuanza kuwagawia masomo kwa ajili ya watoto wao, hali ambayo inaweza kusababisha maambukizo ya ugonjwa huo.

Kwa maana hiyo, kusiwapo na njia nyingine za ujanja za kuwakusanya wanafunzi na kuanza kuwafundisha wakati huu ambao nchi inapambana na virusi vya corona, huku kukiwa na zuio la mkusanyiko wa watu.

Ninasema hivyo kwa sababu, kumekuwapo na madai kwamba baadhi ya watu wakiwamo walimu, walikuwa wakikusanya wanafunzi wanajiandaa kufanya mtihani wa taifa na kufundisha masomo ya ziada.

Kimsingi wanaweza kuwa na nia nzuri, lakini wakati huu wa corona si sahihi, wanaweza kusababisha kuendelea kuenea kwa maambukizo ya ugonjwa huo ambao kwa sasa unaitesa dunia.

Katika salamu zake baada ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Wilaya ya Ruangwa (CWT), mkoani Lindi, Raphael Soko, anawataka walimu wilayani humo kuzingatia maelekezo ya serikali.

Kwamba, baada ya shule kufungwa, baadhi ya walimu wilayani humo, walianza kuwakusanya wanafunzi wanaojiandaa kufanya mtihani wa taifa na kuanza kuwafundisha kimya kimya.

Anakiri kwamba wanafunzi wanatakiwa kuandaliwa kwa ajili ya mtihani wa taifa, lakini kwa sasa ni vigumu kutokana na hatari ya corona, hivyo ni muhimu wanafunzi wabaki nyumbani wakiendelea kujisomea.

Cha msingi anasisitiza kuwa walimu watumie likizo hii ya corona kuwafundisha watoto wao jinsi ya kunawa maji tiririka kila wakati na sabuni wakiwa nyumbani, kuvaa barakoa na kukaa kwa kupeana nafasi ili wazoee.

Anachosema mwalimu huyu ni sahihi kwani walimu wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kutekeleza maagizo ya wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa vitendo.

Ikumbukwe kuwa walimu ni wazazi au walezi, wana nafasi kubwa katika vita dhidi ya corona kwa kutumia njia nyingi za kuwasiliana na wanafunzi wao kuliko kuwakutanisha kwa ajili ya masomo ya ziada.

Kama nilivyosema, kwa sasa baadhi ya shule zinawatumia wanafunzi masomo kwa njia ya mtandao au wazazi na walezi kila mmoja kwa nyakati tofauti kwenda shuleni kufuata masomo hayo kwa ajili ya mtoto wake.

Hivyo njia hiyo na ile ya vipindi vya masomo kwa njia ya redio na televisheni zizingatiwe, huku wazazi na walezi nao wakihakikisha kwamba vipindi hivyo havipiti bure bila kuwa na manufaa kwa watoto wao.

Inawezekana wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao muda mwingi wanautumia kuangalia filamu au kusikiliza vipindi vingine ambavyo vyaweza visiwe na manufaa yoyote ya kielimu kwa watoto wao.

Hao wote wanatakiwa kutambua kuwa vipindi vya masomo vinavyofundishwa kila siku za kazi kuanzia saa tatu asubuhi ni vya muhimu kwa watoto wao kuliko kuangalia filamu au kusikiliza tamthilia.

Jambo la msingi ni watoto kutulia nyumbani wasome au wafuatilie vipindi hivyo katika televisheni au redioni kuliko kuachwa wakicheza kutwa nzima na kujikuta wakiendelea kurudi nyuma wakati huu wa likizo.

Vilevile wazazi na walezi wasitumie televisheni au redio kuweka vipindi visivyoendana na masomo, kwani kwa kufanya hivyo watasababisha watoto wao kushindwa kufuatilia masomo.

## HABARI KITAIFA




Mafundi wakiendelea na ujenzi wa upanuzi na ukuta wa Mto Ng'ombe, eneo la Kijitonyama na Tandale, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Miradi mitano iliyopewa kipaumbele Wizara Ujenzi

**Na Salome Kitomari,**

DODOMA

SERIKALI imepanga kuendelea kutekeleza miradi mikubwa mitano ya kuboresha mawasiliano, uchukuzi na ujenzi mwaka ujao wa fedha.

Akiwasilisha makaridio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Waziri Isack Kamwelwe, alisema miradi hiyo ni ya kipaumbele na ukamilikaji wake utakuwa na matokeo makubwa kwenye sekta nyingine.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni inayoelekea kwenye vivutio vya utalii, bwawa la kufua umeme la Nyerere, ujenzi wa reli mpya ya kisasa, ufufuaji wa Shirika la Ndege (ATCL) na ujenzi na ukarabati wa meli katika maziwa makuu.

Mingine ni madaraja, bandari, viwanja vya ndege, reli na vivuko, miradi ya makao makuu ya nchi kama vile miradi ya barabara za kupunguza msongamano katika Jiji la Dodoma, Uwanja wa Ndege wa Msalato, treni za abiria mijini (commuter trains), nyumba za watumishi wa umma na majengo ya serikali.

Kwa mujibu wa waziri huyo, mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2020/21 ni wa tano na wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 -20/21).

Waziri huyo alisema miradi ambayo washirika wa maendeleo wameonyesha nia ya kutoa fedha za utekelezaji, serikali pia ikitakiwa kutoa mchango wake (Counterpart Fund); miradi ya kimkakati (kama vile ulinzi wa mipakani).

Alisema wizara itaendelea kutekeleza miradi yote kwa uwazi na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma ili kuepusha kuwapo kwa vitendo vya rushwa.

Alisema wizara itachukua hatua stahiki dhidi ya watakaobainika kukiuka sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Kwa mujibu wa waziri huyo, Sh. trilioni 1.577 zinahitajika kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maendeleo ya ujenzi wa barabara, vivuko na nyumba, na majengo mbalimbali kwa kipindi cha mwaka ujao wa fedha. Kati yake, Sh. trilioni 1.252 ni fedha za ndani na Sh. bilioni 325.364 ni za fedha za nje.

Kwa sekta ya uchukuzi, alisema kwa mwaka huo zimetengwa Sh. trilioni 3.062 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Sh. trilioni 2.938 fedha za ndani na Sh. bilioni 124.469 fedha za nje).

Alisema miradi itakayotekelezwa ni kuboresha huduma za usafiri na usalama wa watu na vyombo vya usafiri katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa na viwanja vya ndege.

Mingine kukarabati na kujenga reli ikiamo ununuzi wa vifaa ikiwamo injini tatu na mabehewa 44 ya njia ya reli ya kati iliyopo sasa, kukamilisha kazi ya upembuzi na usanifu wa awali na kuanza ujenzi wa reli ya jijini Dodoma, ununuzi wa vichwa vya treni vitano, mabehewa ya abiria 60, mabehewa ya mizigo 1,430 kwa ajili ya uendeshaji wa SGR; ukarabati wa karakana, stesheni na majengo ya reli iliyopo.

CORONA

Pia, wizara hiyo ilieleza kuwa janga la corona limeathiri utendaji wa bandari na viwanja vya ndege nchini.

"Hali ya corona imeleta hofu kubwa katika Sekta ya Uchukuzi hususan kwenye bandari na viwanja vya ndege hivyo kuathiri utendaji wa taasisi zinazotoa huduma katika maeneo hayo," alisema na kuongeza:

"Wizara inaendelea kuchukua tahadhari katika vituo vya mipakani, viwanja vya ndege na maeneo ya bandari ili kudhibiti maambukizo ya virusi vya corona. vifaa vya kinga vimeendelea kutolewa kwa wafanyakazi katika maeneo hayo pamoja na utoaji wa elimu kwenye vyombo vya usafiri."

Bunge hilo lilipitisha bajeti ya Sh. trilioni 4.96 kwa ajili ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha. Mwaka huu, iliidhinishiwa Sh. trilioni 4.78, hivyo kuna ongezeko la Sh. bilioni 16.

# Chadema yafuatilia wabunge wake

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimesema kinafuatilia kwa karibu hatua ya wabunge wake kukaidi maelezekezo ya Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe ya kuwataka kutohudhuria vikao vya Bunge na kujitenga kwa siku 14 ili kujiepusha na maambukizo ya corona

Akizungumza na gazeti hili , Mkuu wa Idara ya Habari na Uenezi ya chama hicho, Tumaini Makene, alisema jana chama kitatafakari na kutoa majibu ya hatua za kuchukua.

"Chama kinafuatilia kwa karibu suala hilo na kitatafakari uamuzi wa kuchukua dhidi ya wahusika."

Wiki iliyopita, Mbowe alitaoa maelekezo kwa Wabunge wote wa chama hicho kutohudhuria bungeni na kujitenga kwa muda usiopungua siku 14 kwa kile alichosema ni kujizuia na maambukizo ya virusi vya corona ambapo mpaka sasa mbunge mmoja ameshathibitishwa kupatikana na virusi hivyo.

Akinukuliwa na chombo kimojawapo cha habari nchini kuhusu hatua iliyochukuliwa na Kiongozi huyo wa kambi rasmi bungeni ya kuwataka wabunge wa upinzani kutohudhuria vikao hivyo wa bunge la bajeti, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema ni uamuzi wa kibabe kwa wabunge wa chama hicho na kuwa Bunge halijapendezwa na hatua hiyo.

"Wabunge ni timu moja, huwezi kwenda katika timu unatoa tu wachezaji wako tokeni hata hujajadiliana na wenzako," alisema Ndugai.

Juzi Rais John Magufuli, alisema ametoa maelekezo kuwa wabunge watakaosusia Bunge wakatwe mishahara.

# Msako wanaouza sukari bei juu Dar kuanza leo

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amesema kuanzia leo mkoa wake utawakamata wafanyabiashara wanaouza sukari kinyume cha bei elekezi isiyozidi Sh. 2,600 kwa kilo.

Amesema katika ukaguzi wao huo, sukari itakayokamatwa inauzwa kinyume cha maelekezo ya serikali, itataifishwa huku wahusika wakikamatwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Makonda alisema amebaini baadhi ya wafanyabiashara wanauza kilo moja ya sukari kwa Sh. 3,500 badala ya Sh. 2,600 iliyoelekezwa na Wizara ya Kilimo.

Kutokana na hilo, amewaagiza wakuu wa wilaya zote tano mkoa huo kuhakikisha wanafanya ukaguzi wa kuwabaini wafanyabiashara hao ili wakamatwe na sukari hiyo itaifishwe.

"Msako huu unaanza kesho (leo) na asisalie mfanyabiashara yeyote anayeuza sukari kwa bei ya juu," aliagiza.

Makonda alisema hakuna sababu ya kutumia mwezi wa Ramadhani kuwakandamiza watu.

"Sukari yote hata ikiagizwa nje ya nchi, inapita Dar es Salaam haiwezekani mkauza mpaka Sh. 3,500 kwa kilo. Timu ya mkoa imepita, inawafahamu wafanyabiashara wote. Kuanzia kesho (leo) tutaanza kukamata wafanyabiashara na kutaifisha sukari ambayo mnauza bei juu.

"Tumewaambia kwa sababu tunawapenda ili muda huu (jana) mfanye marekebisho lakini kuanzia kesho (leo), Wakuu wa Wilaya Kigamboni, Temeke, Ilala, Kinondoni na Ubungo na timu zenu piteni, kamateni na kuichukua hiyo sukari," aliagiza.

Makonda alisema uongozi wa mkoa huo utaichukua sukari hiyo na kuiuza kwa bei elekezi na fedha itakayopatikana ikatumika kununua vifaa vya kuwakinga madaktari wa Mkoa wa Dar es Salaam.

"Hakuna sababu ya kupimana ubavu, kuuza nje ya maelekezo ya serikali bei inajulikana na serikali ilitoa vibali vya uagizaji nje ya nchi, hakuna sababu ya kupandisha bei na kuwaumiza wananchi," alisema.

Mwezi uliopita, serikali kupitia Wizara ya Kilimo ilitoa bei elekezi ya bidhaa hiyo muhimu. Bei hiyo inanzia Sh. 2,600 hadi 3,200 kwa kilo, ikizingatia jiografia ya mkoa husika.




Mganga Mkuu wa Hospitali ya Temeke, Dk.Gwamaka Mwabulambo (Kulia), akipokea msaada wa lita 250 za vitakasa mikono kutoka kwa meneja wa kiwanda cha Tanzania Distilleries Ltd (TDL), Aranyaeli Ayo (katikati), vilivyotolewa na kampuni hiyo kuunga mkono jitihada za serikali za kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona kwa ajili ya vituo vya afya wilayani humo katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana, kushoto ni Meneja Mawasiliano wa TBL Plc, Amanda Walter. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Ataka wabunge wakatwe posho corona

**Na Salome Kitomari,**

DODOMA

MBUNGE wa Nkasi (CCM), Ally Kessy, amewataka wabunge kuacha kulalamika kuhusu corona na badala yake wachangie kukabiliana na mlipuko wa virusi hivyo kwa kutoa posho zao za siku mbili.

Akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano bungeni jijini hapa jana, Kessy alisema haifai kuendelea kuilaumu serikali bila kuchangia.

"Nimesikiliza wabunge wanalalamika kuhusu utendaji wa serikali kuhusu corona. Nilitarajia tuwe wa kwanza kuchangia, mbona siwaoni mkisema tutoe hata malipo yetu ya siku mbili kwenda kupamba na corona?" Alihoji.

Mbunge huyo alisema wanasikika wafanyabiashara na mashirika mbalimbali wakichangia fedha na vifaa kukabiliana na mlipuko wa virusi hivyo, lakini hakuna wabunge waliosikika wakichangia.

"Badala ya kulalamika, ni vizuri tukaonyesha mfano kwa kuchangia fedha ziende serikalini kwa ajili ya kupambana na corona," alishauri.

Mbunge wa Mtwara Mjini, Maftah Nachuma (CUF), alisema wabunge wa chama hicho hawatatoka bungeni kutokana na mlipuko wa corona, badala yake wataendelea kushiriki hadi mwisho wa Bunge la Bajeti.

"Nimewasiliana na Mwenyekiti wetu, Prof. Ibrahim Lipumba, ambaye ametuelekeza tuendelee kuhudhuria vikao," alisema.

# Bei sukari bado kizungumkuti Kahama

**Na Ndalike Sonda,**
KAHAMA

BAADHI ya wafanyabiashara wa sukari wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wamesema kuwa sukari inayowekwa kwenye vifungashio vya kilo moja imeadimika.

Wamesema kwa zaidi ya wiki mbili haiuzwi madukani kutokana na kutopatikana.

Wakizungumza na Nipashe jana Mjini Kahama, walisema tangu serikali itoe bei elekezi ya Sh. 2,900 kwa kilo moja katika mkoa wa Shinyanga, sukari hiyo imekuwa adimu kupatikana.

Mwita Omari, mfanyabiashara wa sukari, alisema sukari iliyopo kwenye vifungashio yenye kilo 20 ilikuwa inauzwa Sh. 65,000 ambapo ukigawanya kwa kilo moja inauzwa Sh. 3,250, hali ambayo alisema anadhani imesababisha sukari hiyo kuadimika.

Alisema kwa sasa sukari iliyopo ni ile ya kupima ambayo ndio inanunuliwa kwa wingi na wateja, ingawa wanauza bei ya Sh. 3,000 hadi 3,300 tofauti na bei elekezi ya serikali ambayo ni Sh. 2,900 katika mkoa wa Shinyanga.

Kuhusu kuuza kwa bei kubwa zaidi ya iliyoelekezwa na serikali, Mwita alisema inatokana kwa bei ya jumla ya Sh. 73,000 ambayo ukiigawa kwa kg 1 unanunuliwa kwa bei ya Sh. 2,9200, huku mfuko wa kilo 50 unanuliwa kwa bei ya Sh. 140,000, na kwamba serikali itoe bei elekezi kwa wazalishaji na mawala wa sukari nchini.

Mfanyabishara mwingine, ambaye hakutaka kuujitambulisha jina lake, aliiomba serikali kuzalisha sukari ya kutosha ili kuondoa tatizo la kuadimika, na kwamba wakizalisha kwa wingi itasaidia kuendana na bei elekezi ya serikali.

Mkazi wa Nyahanga Neema Willium, alisema kwa sasa katika Mtaa wa Nyahanga wananunua kwa bei ya Sh. 3,200 kwa kilo, na kwamba wanaiomba serikali kuingilia kati ili agizo la bei elekezi itekelezwe na wafanyabiashara kwa kuwa hakuna anayetekeleza.

Aprili 24, 2020, Serikali kupitia kwa Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alitangaza bei elekezi ya sukari kwa kila mkoa nchini, huku akiwaonya watakaobainika kuuza kinyume cha utaratibu huo kuwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ikiwamo kunyang'anywa leseni ya biashara.

# Watu maalum watakiwa usafi karantini corona

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

BARAZA la Madiwani Wilaya ya Wete limeshauri kuandaliwa watu maalum wa kufanya usafi kwenye kambi za karantini ambao wamepewa elimu sahihi na mafunzo ya kujikinga na virusi vya corona.

Wakijadili mapato na matumizi kwa kipindi cha miezi mitatu Januari –Machi, 2020 ya Kamati ya Afya na Mazingira, walisema ni vyema serikali kuu kupeleka watendaji wa Wizara ya Afya kufanya usafi kwenye maeneo ya karantini.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Assaa Juma Ali, alisema pamoja na Baraza kuajiri watu wa usafi, lakini kutokana na janga la ugonjwa wa Covid-19, wanatakiwa kuandaliwa mazingira ambayo yatakuwa ni salama kwao.

Alisema asilimia kubwa ya wafanyakazi wa usafi wa Baraza hawana elimu sahihi ya kujikinga na virusi vya corona, hivyo wanatakiwa kulindwa ili wasipatwe maambukizo.

"Wafanyakazi wa usafi wa Baraza wengi hawana elimu sahihi ya kujikinga na virusi vya corona, hivyo suala la kwenda kufanya usafi kwenye maeneo ya karantini liwe na wafanyakazi wa Wizara ya Afya," alisema.

Naye Diwani wa Wadi ya Kiungoni, Mussa Ayoub, aliushauri uongozi wa Baraza la Mji kwa kushirikiana na serikali ya wilaya kuwapangia wafanyakazi wa wizara ya afya kufanya usafi maeneo ya karantini.

Alisema wakati serikali iko kwenye mapambano ya virusi vya corona, ni vyema wafanyakazi wa baraza nao kupunguziwa majukumu ikiwamo kutopangiwa kufanya usafi maeneo hayo.

"Lazima hawa wafanyakazi wa usafi tuwaangalie kwa jicho la huruma, sehemu za karantini wasipangiwe kwenda kusafisha, hii itasaidia kuwalinda na maambukizo ya virusi vya corona," alieleza.

Mkuu wa Wilaya ya Wete, Kepteni Khatib Khamis Mwadini, alisema katika maeneo ya karantini hakuna mshukiwa wa ugonjwa huo, hivyo wafanyakazi wa usafi wataendelea kutimiza majukumu yao.

**Wafanyakazi wa usafi wa Baraza wengi hawana elimu sahihi ya kujikinga na virusi vya corona, hivyo suala la kwenda kufanya usafi kwenye maeneo ya karantini liwe na wafanyakazi wa Wizara ya Afya**

# Waagizwa kuwalipa wakulima tumbaku

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BODI ya Tumbaku Tanzania imetoa wiki mbili kwa kampuni ya ununuzi wa zao hilo ya Magefa LTD kuhakikisha inawalipa wakulima wa tumbaku zaidi ya dola za Marekani 35,000.

Malipo hayo ni ya msimu wa 2018/19, na imeagizwa kulipa fedha hizo kabla ya kufunguliwa kwa masomo mapya Mei 15, mwaka huu.

Albert Charles, Meneja wa Bodi ya Tumbaku Mkoa wa kitumbaku Kahama, alitoa maagizo hayo wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na ulipaji wa fedha hizo, huku akiwatoa hofu wakulima kuwa watapatiwa stahiki zao kabla ya masoko mapya kufunguliwa.

Alisema wametoa wiki mbili kuhakikisha kampuni ya Magefa imelipa deni hilo kwa wakulima, na imewahakikishia watalipa fedha hizo kwa vyama vya msingi, Ilomelo, Kangeme na Tumaini Amcos ambapo walinunua tumbaku katika masoko yaliyofanyika Machi 2019 zinazokadiriwa kufikia milioni 80.

Hata hivyo, alisema malipo hayo yalichelewa kutokana na kampuni hiyo kutolipwa, baada ya kuuza tumbaku hiyo nje ya nchi na uwapo wa ugonjwa wa Covid 19, ambao umesababisha nchi nyingi kufunga mipaka na kukwamisha kufanyika kwa masoko hayo.

# Wasiojulikana waua mmoja kwa mapanga

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MTU mmoja amefariki dunia papo hapo baada ya kushambuliwa kwa mapanga na watu wasiojuilikana katika Kijiji Cha Nzinza Roho Shengejuu Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Sadi Khamis, alimtaja aliyeuawa ni Daudi Deos Mpangala (40), mkazi wa Shengejuu Wilaya ya Wete.

Alisema kuwa tukio hilo lilitokea Nzinza Shengejuu majira ya usiku juzi, ambapo walifika watu nyumbani kwake na kumwita ili atoke nje na alipotoka tu walimvamia na kumshambulia kwa mapanga.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi pamoja na kuwasaka waliohusika na tukio hilo.



Wakulima wa kikundi cha Kilimo Kwanza cha Kijiji cha Lyasembe, Kata ya Mrangi, wilayani Musoma, mkoani Mara, wakiandaa shamba kwa kutumia jembe la kukokotwa na ng'ombe, ambalo ni miongoni mwa 25 yaliyotolewa hivi karibuni na Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, kwa vikundi vya wakulima ikiwa ni kampeni ya kuhamasisha kuachana na jembe la mkono. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkurugenzi apewa miezi 2 ujenzi jengo la wagonjwa

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Lutengano Mwalwiba, kuhakikisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) unakamilika ndani ya miezi miwili ili kuwawezesha wakazi wa wilaya hiyo kupata huduma ya afya kwa wakati.

Mongella alitoa agizo hilo baada ya kutembelea hospitali hiyo wakati wa ziara yake ya kukagua shughuli za maendeleo wilayani Magu ikiwamo hospitali hiyo.

Miradi mingine aliyoitembelea ni wa maji Magu Mjini, REA Bugabu na Bonde la Kandawe kwa ajili ya kuangalia shughuli za kilimo cha mpunga, na kusema ujenzi huo ukamilike kabla ya Juni 30, mwaka huu.

Jengo linalojengwa katika Hospitali ya Wilaya ya Magu limegharimu Sh. milioni 300, huku likitarajiwa kuwahudumia wakazi wa wilaya hiyo wanaopewa rufani kutoka katika vituo vya afya kufuatia jengo lililopo kutokidhi mahitaji.

"Jitahidi kabla ya kuanza mwaka mpya wa fedha uwe umekamilisha jengo hili...tutamwalika Waziri Mkuu au Rais akiwa anapita atuzindulie jengo letu na wananchi waanze kupata huduma," alisema Mongella.

Mwalwiba alisema Ofisi ya Rais (Tamisemi) iliwapelekea Sh. milioni 200, kwa ajili ya kufanya ukarabati wa jengo la wagonjwa wa nje la zamani, lakini kutokana na uchakavu wake, wakafikiri siyo busara kuweka fedha hizo katika jengo hilo ambalo hata ukarabati wake usingeonekana vizuri, hivyo waliamua kujenga jengo jipya.

Nao baadhi ya wananchi wa wilayani Magu, walisema endapo jengo hilo litakamilika, litawasaidi kupunguza msongamano na kupata huduma kwa haraka.

# Makandarasi waonywa ucheleweshaji miradi

**Na Hamisi Nasiri,** NACHINGWEA

MKUU wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Hashimu Komba, amewaonya makandarasi wote wilayani humo kuhakikisha wanakamilisha kazi zao kwa wakati kabla serikali haijaingilia kati na kuwaondoa kwenye miradi yake.

Komba alitoa angalizo hilo wilayani Nachingwea alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya barabara zilizopo wilayani hapa ambapo aliongozana na wataalamu wa ardhi.

Alisema baadhi ya makandarasi awali walikuwa wakipewa kazi za kutengeneza miundombinu mbalimbali hasa ya barabara na kuitekeleza chini ya kiwango.

Aliwataka makandarasi waliopo Nachingwea kufanya kazi zao kwa ubora unaotakiwa na kuhakikisha kazi hizo wanazikamilisha kwa wakati uliopangwa.

Komba alisema kila mkandarasi ambaye anafanya kazi katika wilaya hiyo ni lazima afanye kazi kuendana na thamani ya fedha zilizotolewa na serikali, na kama atafanya kazi chini ya ubora, serikali itachukua hatua dhidi yake.

"Leo natoa wito kwa makandarasi wote Nachingwea kuhakikisha kazi zenu zinakamilika kwa wakati na mkandarasi ambaye atashindwa kufanya hivyo basi serikali haitamvumilia," alisema Komba.

Alisema serikali kila mwaka kupitia halmashauri imekuwa ikipanga bajeti ya kutosha kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu yake hasa barabara za mjini na vijijini, hivyo mkandarasi ambaye ataonyesha kutaka kukwamisha jitihada hizo serikali haitamfumbia macho.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea kila mwaka wa fedha imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuboresha madhari ya Mji wa Nachingwea, hivyo mkandarasi yeyote ambaye amepewa kazi lazima aifanye kwa uthabiti.

Alisema hakuna sababu yoyote ya msingi ya kuendelea kufanya kazi na makandarasi ambao wamekuwa wakikwamisha ujenzi wa baadhi ya miundombinu kwa sababu watajikuta wakiingia kwenye tatizo kutoka katika mkono wa serikali.

Komba alisema kuwa kila mkandarasi aangalie kazi aliyopewa inakamilika kwa wakati, na kwamba lazima ahakikishe kazi hiyo anaifanya vema na kuimaliza kama mkataba unavyomtaka.

HABARI BUNGENI

# Mabilioni yatengwa kukamilisha maabara






Habari na Augusta Njoji

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imesema mwaka ujao wa fedha, Sh. bilioni 42 zimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara zilizojengwa kwa nguvu za wananchi.

Hayo yalibainishwa bungeni jijini hapa jana na ofisi hiyo ilipojibu swali la Mbunge wa Hanang' (CCM), Dk. Mary Nagu.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema mwaka 2013 hadi 2015, serikali ilihamasisha wananchi kujenga vyumba vya maabara katika shule mbalimbali wilayani Hanang', lakini hadi sasa maabara hizo hazijakamilika.

"Je, serikali ipo tayari kutoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa maabara hizo? " Alihoji.

Katika majibu yake, ofisi hiyo ilisema serikali iko tayari kuunga mkono jitihada za wananchi katika ukamilishaji wa ujenzi wa maabara za shule za sekondari kwa ajili ya masomo ya sayansi.

"Kati ya fedha hizo, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' imeidhinishiwa Sh. milioni 210 ambazo zitatumika kukamilisha maabara saba," ilibainisha.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Magu (CCM), Boniventura Kiswaga, amehoji mpango wa serikali kupunguza Kodi ya Huduma (Service Levy) kutoka asilimia 0.03 hadi 0.01 ili kuleta unafuu kwa wafanyabiashara nchini.

Ofisi hiyo ilijibu kuwa ushuru wa huduma unaotozwa kwa Mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 Kifungu cha 6 (u) na 7(z).

"Kwa mujibu wa sheria hiyo, halmashauri zina hiari na uwezo wa kupanga kiwango cha ushuru wa huduma kisichozidi asilimia 0.3," ilisema.

Hata hivyo, ofisi hiyo ilisema sheria imetoa mwanya wa kupunguza ushuru huo kulingana na mazingira ya biashara, uzalishaji na ulipaji wa kodi katika halmashauri husika.

# Ahoji mpango kuinua pamba



MBUNGE wa Busega (CCM), DK. Raphael Chegeni, amesema zao la pamba limekuwa likikumbwa na tatizo la bei na pembejeo mwaka hadi mwaka.

Mbunge huyo alihoji bungeni jijini hapa jana mpango wa serikali kuwasaidia wakulima ambao badala ya zao kuwaletea tija kiuchumi, limeendelea kuwatia umaskini kutokana na gharama za uzalishaji pamoja na huduma za ugani.

Katika majibu ya Wizara ya Kilimo kwa mbunge huyo, ilielezwa kuwa serikali inachukua hatua mbalimbali kutatua matatizo ya bei, pembejeo na huduma za ugani zinazowakabili wakulima wa zao la pamba nchini ili kuwaondolea umaskini.

"Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha mfumo wa uzalishaji wa mbegu bora za pamba katika maeneo ya Igunga na Kasekese katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi na kusajili wakulima wote wa pamba kwa ajili ya kurahisisha uratibu na kuwawezesha kupata pembejeo za zao la pamba," ilisema.

Wizara hiyo ilibainisha kuwa serikali inaendelea kuratibu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima wa pamba kwa kuagiza viuadudu kwa mfumo wa pamoja.

"Mfumo huo utasaidia kupatikana kwa viuadudu kwa wingi, vyenye ubora wa hali ya juu, kwa wakati na vyenye bei nafuu ili kuongeza uzalishaji na tija," ilisema.

Wizara hiyo ilibainisha kuwa hadi kufikia Desemba 2019, jumla ya tani 31,955 za mbegu za pamba zilikuwa zimesambazwa kwa wakulima katika wilaya zote zinazolima zao hilo.

Pia, ilisema hadi Machi mwaka huu, chupa za viuadudu 2,454,602 kati ya lengo la chupa 4,000,000 zilikuwa zimekwishasambazwa kwa wakulima.

"Serikali imeendelea kupanua wigo wa utoaji wa huduma za ugani kwa kufundisha wakulima wawezeshaji (Lead Farmers) 4,532 na kuwajumuisha na mtandao wa maofisa ugani uliopo ili kuwafikia wakulima wengi katika maeneo yao," ilisema.

Wizara hiyo pia ilisema serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na wabia wa maendeleo, imeendelea kuboresha huduma za ugani kwa kuwapatia usafiri wa pikipiki maofisa ugani.

"Maofisa ugani 27 wamepatiwa usafiri huo na magari kwa maofisa ugani 13 wa Bodi ya Pamba walioko katika wilaya zinazozalisha zao la pamba ili kuboresha utoaji huduma za ugani kwa wakulima," ilisema.

Wizara hiyo pia ilisema ni matarajio ya serikali kuwa juhudi zote hizo zitapunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija kwa zao la pamba kutoka kilo 300 hadi kufikia kilo 1,000 kwa ekari na hivyo kupunguza umaskini kwa wakulima wa pamba.



## Wanafunzi 3,800 wapata mimba mwaka mmoja

BUNGE limeelezwa kuwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2019, wanafunzi 2,839 wamepewa mimba na 1,244 walirubuniwa na kukatizwa masomo yao.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilipojibu swali la Mbunge wa Ileje (CCM), Janeth Mbene.

Akijenga swali lake, mbunge huyo alisema hivi karibuni kumejitokeza suala lililozua mjadala mkubwa kuhusu wanafunzi kupata mimba na kusababisha kukatisha masomo yao.

"Mwaka 1998, Bunge lilipitisha sheria maalum ya makosa ya kujamiiana (SOSPA) ambayo ilibadili sheria kadhaa na kuweka sheria inayoshughulikia makosa ya udhalilishaji wa kingono na wa kijinsia iliyolenga kurudisha heshima, usalama na hadhi ya wanawake na watoto," alisema.

Alihoji idadi ya watu ambao mpaka sasa wametiwa hatiani na kufungwa kifungo kilichoainishwa kwenye sheria hiyo.

"Je, kati ya watu waliofungwa, watu wazima ni wangapi, na wanafunzi waliowapa mimba wanafunzi wenzao ni wangapi na wako wapi kwa sasa?

"Je, kati ya watoto waliopo shuleni na ambao hawapo shuleni, ni wangapi waliobakwa au kurubuniwa na wangapi waliofanya nao mapenzi kwa hiari?" Alihoji.

Katika majibu yake, wizara hiyo ilisema mpaka sasa jumla ya watuhumiwa 456 wamekwishatiwa hatiani kwa makosa hayo, kwa mujibu wa Sheria ya SOSPA na kufungwa kwa makosa hayo na kwa mujibu wa sheria hiyo.

"Watu wazima ni 373 na wanafunzi waliowapa mimba wanafunzi wenzao ni 83. Takwimu za hivi karibuni, zinaonyesha kwamba katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2019 jumla ya wanafunzi 2,839 walipewa mimba na wanafunzi 1,244 walirubuniwa na kukatizwa masomo yao," ilisema.

Vilevile, wizara hiyo ilisema katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu, jumla ya watoto 892 walibakwa na 133 walirubuniwa na kukatizwa masomo yao.

"Kesi zote hizo zipo katika hatua mbalimbali za kisheria ambapo zingine zimekwishatolewa hukumu na zingine ziko katika hatua mbalimbali za kiupelelezi," ilisema.

Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 5, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 12

## Utaratibu huu ungewezesha kupata mafao kwa wakati



Ukurasa 14

## Kutii maelekezo kuacha hofu, silaha ya corona




Ukurasa 13

Corona yachochea njaa Afrika Congo, Nigeria, Sudan kusota

ELIMU

## NA SABATO KASIKA

# Ndivyo jamii inavyojipanga kuongeza madarasa 2021

LICHA ya kuwapo na hofu ya corona ambayo imesababisha wanafunzi kuwa likizo, jamii katika Halmashauri ya Musoma mkoani Mara, imeanza kujenga madarasa ili kupokea wanafunzi wapya 2021.

Mwaka 2016, ndiyo ambao Watanzania walianza kufurahia matunda ya elimu bure, baada ya serikali kuanza kugharamia elimu shule za msingi hadi kidato cha nne, ikiwa ni njia mojawapo ya kupunguzia wazazi mzigo.

Lakini pamoja na kufurahia matunda hayo, kuna changamoto ya uhaba wa madarasa ambayo inaendelea kuzikumbuka shule hizo kila mwaka na kusababisha wanafunzi walundikane katika vyumba vichache.

Imekuwa ni kawaida kwenye baadhi ya mikoa kusikia wanafunzi waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza kuanza masomo kwa mafungu huku wengine wakisubiri ujenzi wa madarasa ukamilike.



Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Kiemba, katika halmashauri hiyo, wakisomba maji kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya Shule ya Msingi Murunyigo. **NA MPIGA PICHA WETU**

Changamoto hiyo imesababisha baadhi ya wazazi kuivalia njuga ili kuhakikisha kwenye maeneo hayo hakuna uhaba wa madarasa kila mwaka kama ambavyo imekuwa ikijitokeza na kuleta usumbufu kwa wanafunzi.

Wazazi hao ni wa vijiji vilivyo ndani ya Halmashauri ya Musoma mkoani Mara, ambao baadhi yao sasa wanajenga madarasa kwa ajili ya wanafunzi wanaotarajia kuanza kidato cha kwanza mwaka 2021.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, John Kayombo, anasema, kule ambako ujenzi wa madarasa ya kidato cha kwanza mwaka huu umeshakamilika, wameanza kujenga ya kidato cha kwanza kwa mwaka 2021.

"Wakazi wa Kata ya Busambara yenye vijiji vitatu wameonyesha mfano huo kwani sasa wanajenga madarasa kwa ajili ya wanafunzi watakaoanza kidato cha kwanza mwaka ujao wa 2021," anasema Kayombo.

Anavitaja vijiji hivyo kuwa ni Maneke, Mwiringo na Kwikuba, ambavyo wakazi wake wamegawana majukumu ya kujenga madarasa ya Busambara Sekondari iliyoanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka huu.

### MADARASA

Mkurugenzi huyo anasema, wakazi hao wanajenga madarasa sita, hivyo kila kijiji kinajenga mawili na kwamba wakazi wa kijiji cha Maneke wanajiandaa kumalizia boma la vyumba viwili.

"Kwa upande wa wakazi wa Kwikuba ni kwamba wako mbioni kuanza ujenzi wa vyumba viwili, kwa sasa wanafyatua matofali, wakati wenzao wa Mwiringo wanaendelea kusomba mchanga nao wajenge," anasema.

Anaeleza kuwa sasa ni awamu ya pili ya uchangiaji na ujenzi wa Busambara Sekondari, na kwamba awamu ya kwanza ilihitimishwa mwaka jana, huku nguvukazi ya wananchi na fedha taslimu vikiwa na thamani ya Sh.milioni 45.

"Serikali kuu ilitoa Sh. milioni 37.5, hivyo tunaishukuru lakini pia halmashauri mbali na kusimamia manunuzi kupitia fedha za mfuko wa jimbo, imechangia masinki 14 ya vyoo na Sh. milioni mbili," anasema.

Anafafanua kuwa, mwaka ujao, Busambara Sekonadari inatarajia kupokea wanafunzi 270 wa kidato cha kwanza licha ya kwamba kuna corona hayo ndiyo matarajio yao, hivyo wazazi wameona washiriki mapema kujenga vyumba vipya huku halmashauri ikiwaunga mkono.

Kayombo anasema, halmashauri yake inaendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya shule kwa kutambua kuwa shule hizo ni mali yao, hivyo hawana budi kuzihudumia.

### IDADI YA SHULE

Akizungumzia shule, mkurugenzi huyo anasema, halmashauri yake ina shule 111 za msingi na 20 za sekondari ambazo zote ni za serikali, na kwamba wananchi wanashirikiana na serikali katika uboreshaji wa shule hizo.

"Kama unakumbuka, mwishoni mwa mwaka jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliagiza ujenzi wa madarasa ukamilike mapema ili wanafunzi wote wa kidato cha kwanza mwaka huu waanze masomo kwa pamoja," anasema.

Anasema, lengo la serikali la kutaka wanafunzi wote wanaanze kusoma kwa pamoja ni kwa sababu wakipishana muda wa kuanza masomo baadhi yao wanashindwa kufanya vizuri jambo ambalo si sahihi.

"Hivyo katika halmashauri yetu tumejitahidi kujenga madarasa kwa ajili ya kidato cha kwanza kwa mwaka huu na pia baadhi ya maeneo wameanza ujenzi wa madarasa mengine kwa ajili ya kidato cha kwanza mwaka ujao," anasema.

Anasema, juhudi za kuhamasisha wananchi kushiriki ujenzi na uboreshaji wa miundombonu ya shule unaendelea kuanzia msingi hadi sekondari na kwamba wapo baadhi wamepiga hatua hadi kujenga sekondari ya kijiji.

"Kwa hiyo tunakwenda vizuri ingawa kwenye wengi huwa kuna changamoto zake, lakini mwitikio wa wananchi mzuri, wanaunga mkono juhudi za halmashauri yao na serikali kwa ujumla," anasema.

### KUTOA HAMASA

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Busambara, Victor Kasyupa, anasema, ujenzi wa madarasa mapya ya Busambara Sekondari kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2021 unahusisha pia wazaliwa wa kata hiyo wanaoishi mikoani.

Kasyupa anawataja baadhi yao kwa majina ya Joseph Chikongoye, Wakili Saidi Chiguma, Richard Cheumbe na Thadeo Makindu ambao pia wanachangia posho za kila mwezi za walimu wa kujitolea.

"Tunawashukuru pia kwa hatua hiyo yenye lengo la kuinua elimu kwenye kata yao, kwani wazaliwa hao 13 wa vijiji hivyo waishio maeneo mbalimbali nchini, wamechangia Sh. milioni 1.2, shule hiyo ina walimu wawili wa kujitolea ambao wanalipwa posho na wazaliwa hao," anasema Kasyupa.

Ofisa Mtendaji huyo anasema, mbali na wazawa hao, mbunge wa jimbo Profesa Sospeter Muhongo, naye amechangia mifuko 150 ya saruji, mabati 112 na kupaka rangi vyoo vyote.

ELIMU

NA REUBENI LUMBAGALA

# Utaratibu huu ungewezesha kupata mafao kwa wakati



Wastaafu wakifurajia maisha bora baada ya kazi ya utumishi wa umma . Furaha inategemea kupata pensheni kwa wakati. **PICHA: MTANDAO**

MOJA ya haki ya msingi ya mtumishi ni kupata mafao yake amalizapo muda wa utumishi.

Mafao ya mtumishi yanajumuisha michango aliyochangia kupitia makato ya mshahara wake pamoja na mchango wa mwajiri wake ambayo kwa pamoja huchanganywa na kumpatia mwajiriwa mafao.

Ni malipo muhimu kwani humsaidia mtumishi kuendesha maisha yake baada ya kumalizika muda wa utumishi wake kwenye kampuni, taasisi au serikalini.

Ipo changamoto kwa baadhi ya wastaafu kucheleweshewa mafao yao. Hii imesababisha baadhi yao kuishi maisha magumu baada ya kustaafu na hivyo kujikuta wakiingia kwenye madeni kufuatia kukopa maeneo mbalimbali kama taasisi za fedha na baadhi huwatoza riba kubwa hivyo kuwafanya wastaafu kulipa fedha nyingi baada ya kupata mafao yao na kubaki na salio kiduchu.

Upo utaratibu uliowekwa na serikali mathalani kwenye halmashauri, ambao maofisa utumishi wanapaswa kuwasilisha taarifa za wastaafu waliopo kwenye halmashauri zao miezi sita kabla ya kustaafu ili utaratibu wa malipo ya mafao uanze kufanyika, hatimaye muda wa kustaafu utakapofika, aweze kupata mafao yake kwa wakati na maisha baada ya kustaafu yaendelee.

> “ Ni wajibu wa mtumishi kuzifahamu sheria na kanuni za utumishi ili kusimamia na kupata haki zake kwa wakati.

Akiwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya fedha 2020/2021, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, alisema wizara yake imepanga kukutana na maofisa utumishi wote nchini ili kuwakumbusha na kuwasisitiza umuhimu wa kuwasilisha taarifa za wastaafu wizarani miezi sita kabla ya kustaafu ili wapate mafao yao kwa wakati.

Ni jambo linalowaumiza watumishi waliotumikia serikali au sekta binafsi na taifa kwa ujumla kwa weledi mkubwa kucheleweshewa mafao yao na kufikia hatua hata baadhi yao kufariki bila kupata stahili zao.

“Ninasononeka na kitendo cha wastaafu walioitumikia nchi kwa uadilifu na uzalendo kucheleweshewa mafao yao kwa muda mrefu, kuanzia mwaka mmoja hadi minne na wengine kufariki bila kupata mafao yao” anasisitiza Mkuchika.

Dhamira ya serikali kuandaa mkutano na maofisa utumishi ili kuwakumbusha wajibu wao wa kuepuka makosa ya kuchelewesha taarifa za wastaafu ni njia ya kuhakikisha kuwa tatizo la kuchelewa mafao ya watumishi linashughulikiwa na kumalizika.

Ikumbukwe kuwa mafao si hisani bali ni haki ya mtumishi ambayo inajumuisha jasho lake kupitia michango aliyochangia na ile mwajiri aliyomwongezea na ongezeko linalotokana na faida iliyopatikana baada ya uwekezaji kwenye mifuko ya mafao ya kijamii inayotunza fedha za waajiriwa, hivyo kuchelewesha mafao ni ukiukwaji wa haki za watumishi.

Wizara ya Utumishi inategemea kupokea taarifa za wastaafu kutoka kwa maofisa uajiri ili utaratibu wa kuandaa malipo hayo uanze.

Hivyo basi, ikiwa maofisa utumishi watachelewesha au watashindwa kuwasilisha taarifa za wastaafu, ni dhahiri mafao yatachelewa au mtumishi kushindwa kupata mafao hayo.

Upo msemo wa kisheria kuwa “haki iliyocheleweshwa, ni haki iliyokiukwa” (Justice delayed is justice denied), hivyo, suala si watumishi kupata mafao yao bali wayapate mafao yao kwa wakati kwani kuchelewesha haki ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Maofisa utumishi watimize wajibu wao wa kuhakikisha hawawi sehemu ya kuwasababishia watumishi shida ya kucheleweshewa mafao yao bali kuwa sehemu ya kutimiza wajibu wao wa msingi wa kuwasilisha taarifa mapema ili taarifa hizo zishughulikiwe.

Aidha, wanawajibika kufuatilia changamoto za kuchelewa mafao ya watumishi waliopo kwenye halmashauri zao badala ya kuwaachia wastaafu kazi ya kufuatilia madai yao kwani kazi hii huwaongezea wastaafu mzigo wa gharama za nauli, chakula na malazi. Kama ambavyo mtumishi alivyokuwa akitimiza wajibu wake ipasavyo katika utumishi wake, ndivyo ambavyo maofisa utumishi na serikali wawajibike kwa wakati kumpatia mstaafu mafao yake ili afurahie matunda ya utumishi wake.

Vilevile, waajiri wana wajibu wa kuwasilisha michango ya watumishi wao kwa wakati kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kwani ni kupitia michango hiyo ndiyo inayowezesha kupatikana fedha za mafao.

Kushindwa kuwajibika kikamilifu kwa waajiri kunachangia kuzorotesha upatikanaji wa mafao ya watumishi. Hivyo basi, waajiri wahakikishe kila mwezi wanawasilisha michango kwenye mamlaka husika kama njia ya kutimiza wajibu wao muhimu.

Pamoja na umuhimu wa maofisa utumishi kuwasilisha taarifa za wastaafu miezi sita kabla, watumishi wenyewe wawe sehemu ya kuisimamia sheria hii kwa wenyewe kuanzisha na kufuatilia mchakato wa kuandika barua ya kustaafu badala ya kusubiri kupewa taarifa na waajiri wao.

Ni wajibu wa mtumishi kuzifahamu sheria na kanuni za utumishi ili kusimamia na kupata haki zake kwa wakati.

Naamini mkutano na maofisa utumishi ni mwanzo wa kumaliza tatizo la kuchelewa mafao ya wastaafu ambao ni kama wanabebeshwa mzigo mara mbili.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: 0764- 666349***

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Corona yachochea njaa Afrika Congo, Nigeria, Sudan kusota

JANGA la COVID-19 ni wazi linaongeza hatari ya kutokuwa na uhakika wa chakula duniani na baadhi ya mataifa ya Afrika yanayoathirika ni pamoja Congo DRC, Sudan, Sudani Kusini na Nigeria.

Ripoti mpya inayotolewa na mashirika ya Umoja wa Mataifa, Muungano wa Ulaya na Shirika la Marekani la Msaada wa Kimataifa (USAID), inaonyesha kwamba janga la mlipuko wa virusi vya corona au COVID-19 linaweka njia panda mustakabali wa chakula na lishe duniani.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa mlipuko wa virusi vya corona au COVID-19 utasababisha njaa.

Pamoja ripoti hiyo, aidha inasema kuwa, pamoja na kila mwaka kuwa na mgogoro wa chakula na lishe, ripoti nyingine ya wadau iliyotolewa na muungano wa mashirika ya Umoja wa Mataifa, serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayoshughulikia mzizi wa njaa na lishe, inasema COVID-19 inatoa tishio jipya katika uhakika wa chakula na lishe.

Shirika hilo ya Umoja wa Mataifa la mpango wa chakula duniani WFP, jingine la kuratibu misaada ya kibinadamu na masuala ya dharura OCHA, lile la kuhudumia watoto UNICEF, la chakula na kilimo FAO, EU na USAID yanasema ripoti hiyo iliyopewa jina "muungano wa kimataifa dhidi ya mgogoro wa chakula" inaonyesha kwamba mwishoni mwa mwaka 2019 watu milioni 135 katika nchi 55 walikabiliwa na changamoto ya kutokuwa na uhakika wa chakula.




Rais wa FAO, Qu Dongyu, akizungumzia tatizo kukosekana chakula. **PICHA: MTANDAO**

**WATOTO HATARINI**

Na zaidi ya hapo "katika nchi 55 zenye mgogoro wa chakula zilizochunguzwa kwenye ripoti hii watoto milioni 75 walikuwa na matatizo ya kudumaa na milioni 17 waathirika la kupoteza uzito kutokana na utapiamlo kwa mwaka 2019."

Ripoti hiyo inasema hiki ni kiwango cha juu sana cha kutokuwa na uhakika wa chakula na utapiamlo kilichoorodheshwa na mtandao huo tangu kutolewa kwa ripoti ya kwanza mwaka 2017.

Mwaka huohuo wa 2019 ripoti imewaweka watu milioni 183 katika daraja la pili la kutokuwa na uhakika wa chakula ambalo ni sawa na kukabiliwa na njaa kubwa na kuwa katika hatihati ya kutumbukia katika mgogoro wa chakula endapo watakabiliwa na zahma nyingine kubwa kama janga la COVID-19.

Zaidi ya nusu ya watu hao ambao ni milioni 135 walioangaziwa katika ripoti hiyo wanaishi barani Afrika, milioni 43 Mashariki ya Kati na Asia, na milioni 18.5 Amerika ya Kusini na Caribbea.

Nchi 10 zilizoathirika vibaya na uhaba wa chakula mwaka 2019 ni pamoja na Yemen, Congo DRC, Afghanistan, Venezuela, Bolivia, Ethiopia, Sudan Kusini, Sudan, Nigeria na Haiti.

> Hatua za pamoja zinahitajika miongoni mwa wadau wa masuala ya kibinadamu, maendeleo na amani kushughulikia mizizi ya tatizo sugu la kutokuwepo kwa uhakika wa chakula.

Kichocheo kikubwa cha hali hii ripoti inasema ni pamoja na vita ambavyo vimewasukuma watu milioni 77 kwenye hali mbaya ya kutokuwa na uhakika wa chakula, mabadiliko ya tabia nchi yaliyowaathiri watu milioni 34 na kuyumba kwa uchumi ambayo kumewaacha watu milioni 24 bila uhakika wa chakula.

Ripoti imependekeza kuchukuliwa hatua madhubuti hivi sasa ili kuwaepusha watu milioni 265 kutoka katika nchi za kipato cha chini kutumbukia katika janga kubwa zaidi la kutokuwa na uhakika wa chakula.

Na katika kikao maalum cha Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kilichofanyika kutathimini migogoro na uhakika wa chakula, Mkuu wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), David Beasely, anasema "Dunia sio tu kwamba inakabiliwa na janga la kimataifa la afya lakini pia janga la kimataifa la kibinadamu."

Anaongeza kuwa: "Ukweli ni kwamba muda unatutupa mkono, hivyo hebu na tuchukue hatua kwa busara na kwa haraka. Ni muhimu sana kuja pamoja kama jumuiya ya kimataifa kupambana na janga hili la COVID-19"

Anasema janga hilo limesababisha mgogoro mkubwa wa kibinadamu tangu vita vya pili vya dunia hasa ukizingatia kwamba dunia tayari inakabiliwa na dhoruba kubwa kuanzia mabadiliko ya tabianchi, majanga ya asili, vita , njaa na mengineyo.

**OMBI LA MSAADA**

WFP imeliomba Baraza la Usalama kuongoza njia kadhaa katika juhudi za kimataifa kupambana na COVID-19.

Njia hizo ni pamoja na mosi kipaumbele cha kuhakikisha kuwa kunakuwa na amani.

Anawataka wote wanaohusika katika mapigano kuruhusu na kutoa fursa kwa wahudumu wa misaada ya kibinadamu kuzifikia jamii zisizojiweza na kuratibu msaada wa kuokoa maisha pamoja na dola milioni 350 za ufadhili mpya ili kuweka mtandao wa kiufundi kuhakikisha mnyororo wa kimataifa wa usambazaji msaada unaendelea.

Beasley pia anaelezea haja ya kuwa na mfumo wa tahadhari ya mapema akisema: "Endapo hatutojiandaa na kuchukua hatua sasa kupata fursa ili kuepuka pengo la ufadhili na usumbufu katika biashara huenda tukakabiliwa na baa la njaa kama lililoelezwa kwenye biblia katika miezi michache ijayo.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la FAO, Qu Dongyu, anaeleza jinsi ripoti ya kimataifa ya mgogoro wa chakula ya 2020 ilivyo na uhusiano na migogoro .

Anasema "hatua za pamoja zinahitajika miongoni mwa wadau wa masuala ya kibinadamu, maendeleo na amani kushughulikia mizizi ya tatizo sugu la kutokuwepo kwa uhakika wa chakula."

Anaeleza kuwa utabiri wa uhakika wa chakula 2020 si mzuri na hivyo ni muhimu kuwa na tahadhari ya mapema na kuchukua hatua haraka kuzuia kutokuwa na uhakika wa chakula kunakosababishwa na migogoro.

Licha vita, majanga ya asili, mdororo wa kiuchumi na sasa COVID-19 vinavyowasukuma watu kutumbukia katika hali ya kutokuwa na uhakika wa chakula . Dongyu ana matumaini kwamba "Kwa kufuatilia kwa karibu mwenendo wa mabadiliko haya tunaweza kuchukua hatua mapema na kupunguza athari zake." **UN NEWS**

UCHAMBUZI

NA DK. FELICIAN KILAHAMA



Kuvaa barokoa, kunawa mara kwa mara na kukwepa mikusanyiko ni mambo yanayokuepusha na corona. **PICHA: MTANDAO**

# Kutii maelekezo kuacha hofu, silaha ya corona

NIANZE kwa kumshukuru Mungu ambaye ndiye msingi wa yote, anaweza yote na ndiye Alfa na Omega au mwanzo na mwisho, ndiye anayemjaalia kila mmoja uzima na maisha kutokana na hili janga la corona ambalo limesababisha hofu kila upande.

Watanzania wengi tumekumbwa na hofu hiyo inayotokana na kuwapo virusi vya corona. Kupitia taarifa zinazotolewa na vyombo vya habari ikiwamo redio, runinga na magazeti pamoja na mitandao ya kijamii pia kupitia huduma za intaneti; tumeona, kusoma na kusikia jinsi virusi-corona vilivyoitikisa dunia nzima.

Hofu, mashaka na msongo wa mawazo vilichukua nafasi yake kupitia taarifa mbalimbali zilizotufikia baada ya kuona nchi zilizoendelea sana na zenye nguvu kubwa kiuchumi, kiafya na kijeshi; kushindwa kudhibiti kuenea kwa kasi virusi-corona na kusababisha watu wengi kupata maambukizo ya homakali ya mapafu na pia baadhi ya watu kupoteza maisha yao.

Kutoka nchini China ambako tulikuwa tukisikia kuwa virusi corona vilizuka mwishoni mwa mwaka 2019, vikasambaa kwa kasi kubwa hata kufika nchini kwetu na leo zaidi ya watu 400 wameambukizwa ni janga ambalo huongeza hofu.

Baada ya kuona janga hili limetukumba serikali ilichukua hatua za haraka kwa nia ya kuhakikisha maambukizo yanadhibitiwa ipasavyo. Vilevile, wataalam wa afya wamekuwa wakielimisha juu ya umuhimu wa kuchukua tahadhari kubwa kuepuka maambukizo.

> Pamoja na hatua hizo, lakini maambukizo yameendelea kwa kasi kiasi cha kusababisha hofu kubwa kwetu. Kusema kweli wengi wamejaa hofu kubwa ndani mwao.

Pamoja na hatua hizo, lakini maambukizo yameendelea kwa kasi kiasi cha kusababisha hofu kubwa kwetu. Kusema kweli wengi wamejaa hofu kubwa ndani mwao. Kwa nini? Sababu ni COVID-19 kuenea sana, lakini pia haina dawa wala chanjo inayoaminika, hivyo anayekumbwa na virusi hivyo anakuwa na hofu kuwa atakufa.

### CHANZO CHA KUHOFU

Kwa kweli kuwa na hofu ndani ya mioyo yetu siyo jambo jema: maana ni hali hatarishi kwa maisha yetu. Mwenyezi Mungu alivyomuumba mwanadamu wa kwanza na kumuweka katika Bustani ya Eden, alimbariki akampa mamlaka ya kumiliki na kutawala vitu vyote isipokuwa kutokula "matunda" ya mti uliowekwa katikati ya Eden. Hivyo Adam alipewa sharti moja tu la kutochuma matunda ya mti huo na kuyala. Baada ya kushirikiana na mwenzake na kula matunda hayo ikawa mwanzo wa hofu kwao na kwetu.

Kwa nini Adam alijificha? Ni matokeo ya hofu iliyomjaa, akaogopa asijue la kufanya maana moyo wake ulijeruhiwa. Sasa tumekumbwa na hofu ya ugonjwa COVID-19 kiasi cha kusababisha msongo wa mawazo mengi kuhusu hatima ya maisha yetu. Moyo ukijeruhiwa, hofu ikatanda mauti inayemelea. Kwa upande mwingine tujiulize kwa nini tuwe na hofu kiasi cha kuhatarisha maisha yetu wakati tunaye muumba wetu ambaye ndiye chimbuko la yote? Mungu wetu ni mwema na kila mara anatutakia mema hatatuacha tuangamie kupitia COVID-19.

Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia Rais John Magufuli, ambaye anajitahidi kuwatia moyo Watanzania akisema tujipe moyo kwani akili na mawazo mengi vimesheheni woga, kukata tamaa na kujaa hofu ya mauti ndani mwetu kutokana na COVID-19 hasa katika jiji la Dar-es-Salaam.

Kinachotakiwa ni kuondokana na hofu ambayo imetanda miongoni mwetu. Vilevile, tuondoe akilini mwetu kuwa kila anayeambukizwa virusi-corona wanakufa, siyo kweli maana wengi wanapona hata kama dawa haipo lakini aliyetuumba yupo na ndiye kimbilio letu tena anatupigania. Kama tunamjua aliyetuleta duniani kuwa ndiye peke yake mwenye nguvu na uwezo wa kuvisambaratisha virusi-corona Watanzania tuseme nini juu ya hali hiyo?

Ni wazi kuwa tuendee bila kuchoka kumwomba Mwenyezi Mungu atukirimie huruma yake na kuturehemu na kutuepusha na virusi vya corona kwa niaba yetu. Wamtumainio Mungu ni sawa na Mlima Sayuni usiotikisika kamwe.

Ndugu, ulinde sana moyo wako kwa kuondoa hofu na jipe moyo kuu tutashinda na dunia itashangaa hakika Mungu wetu mwema. Virusi-corona si lolote mbele za Mungu maana yeye hakuna linalomshinda.


Kupitia Neno la Mungu mandika yanasema "Kwa kuwa hakuna neno lisilowezekana kwa Mungu" iweje sasa tuingiwe hofu wakati yeye Mungu ndiye aliyetuumba kwa mfano wake? Changamoto hii pia imejitokeza majira ya kusherekea Pasaka kwa Wakristo waliokuwa wakikumbuka kuteswa, kufa na hatimaye kufufuka kwa Masiha Yesu Kristo.

Hakuna haja ya kuhofu maana maandiko yanatuambia kuwa imekwisha na kwamba tuwe na amani mioyoni mwetu.

Hivyo, nguvu ya mauti imegaragazwa ili tuishi kwa amani na bila hofu yoyote. Mwaka 2020 ulipoanza tulisema ni mwaka wenye matumaini ili yaliyoshindikana kufanyika yafanyike bila hofu wala kukata tamaa. Kwa misingi huyo, tuwe na imani kuwa virusi-corona visitutie hofu bali tumuungamie Mwenyezi Mungi dhambi na makosa yetu na kama taifa tumwombe azidishe rehema zake kwetu na kutuondolea balaa la ugonjwa wa COVID-19.

Janga hili litapita na maisha yataendelea lakini tukimtanguliza sana Mungu na kudumu katika kuomba na kumtukuza Mungu wetu kwa kuturehenu na kutukingia hatari zote, kiroho na kimwili. Pamoja na kumtanguliza Mungu, imani thabiti na kutokuwa na hofu kuhusu COVID-19 ni muhimu kuzingatiwa.

Vilevile, inabidi tuenende na kutenda kama tunavyoelekezwa na wataalam wa afya na viongozi wa Serikali. Maana ya kusema Mungu kwanza na mengine yafuate ni kuonyesha kuwa yeye ndiye mponyaji mkuu pia ndiye mwenye hatimiliki ya uhai na maisha yetu hivyo atatuhuisha. Hakika mapenzi yake Mungu yatimizwe katika taifa letu sasa na hata milele.





# Kanisa lawapa angalizo kinamama wenye watoto

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KANISA la Pentecost Maombezi Tanzania limewataka kinamama wenye watoto wachanga wanaonyonyesha kuacha utamaduni wa kuwapa watu wengine wawabebea katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Covid-19, kwa kuwa wanaweza wakaambukizwa na virusi vya corona.

Tahadhari hiyo ilitolewa na Askofu Mkuu wa Kanisa la Pentecost Maombezi Tanzania, Living Mwambapa, alipokuwa akihubiri kwenye ibada iliyofanyika makao makuu ya kanisa hilo Kikuyu Itega mkoani Dodoma.

Alisema kuwa katika kipindi hiki ambacho kuna hatari ya ugonjwa huo wa hatari wa corona, ni vema kinamama wenye watoto wachanga wakachukua tahadhari hiyo ya kuacha tabia waliyoizoea ya kupokezana watoto.

"Nawaomba kinamama wote wenye watoto wachanga, mnatakiwa kuchukua tahadhari kubwa kwa watoto wenu, msiwape watoto wenu watu wengine ili wawapokee... maana hata hao mnaowapa wanaweza kuwa na virusi vya corona, na kuwaambukiza," alisema.

Askofu huyo alisema kuwa ili kujikinga kwa upande wa kinamama wenye watoto ni muhimu wakazingatia na kuchukua tahadhari zaidi ya kuwalinda kwa kutowapa watu wengine na kusababisha maambukizi kwa watoto wao.

Katika hatua nyingine, askofu huyo aliipongeza serikali kwa kuwapiga maarufuku watu wanaopotosha kuwa wameipata dawa inayoweze kuponyesha ugonjwa huu wa corona wakati gonjwa hilo halina dawa wala chanjo.

Aliwataka Watanzania kutodanganywa na taarifa zinazosambazwa na watu hao, ambao wanapotosha kuwa kuna dawa ambayo wameipata inayoweza kuuponya ugonjwa huo.

Aidha, aliwataka waumini wa madhehebu ya dini kuwa na maombi yenye dhamira ya kumgusa Mungu.

Pia aliwataka waumini wa kanisa hilo kuhakikisha wanachukua hatua ya tahadhari kwa wao wenyewe na familia wanazoishi nazo kwa kufuata maelekezo yanayotolewa na viongozi na wataalamu wa afya, huku wakiongeza juhudi zaidi katika maombi.

**Nawaomba kinamama wote wenye watoto wachanga, mnatakiwa kuchukua tahadhari kubwa kwa watoto wenu, msiwape watoto wenu watu wengine ili wawapokee... maana hata hao mnaowapa wanaweza kuwa na virusi vya corona, na kuwaambukiza**

# CCT yaishauri serikali kutoa majibu wanaokufa kwa corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JUMUIYA ya Kikrito Tanzania (CCT) imeishauri serikali kutoa majibu ya watu wanaokufa kwa vifo vinavyotokana na ugonjwa wa corona kwa ndugu zao kwa wakati ili kuondoa maswali ambayo yamekuwa yakijitokeza.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Mchungaji Canon Moses Matonya, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, juu ya patano la viongozi wakuu wa makanisa wanachama wa CCT kuhusu nafasi yao katika kupambana na corona.

Canon Matonya pia alisema jumuiya hiyo inaitaka serikali iendelee kutoa taarifa sahihi kwa wakati ili kusaidia watu kuujua ukweli wa hali ya maambukizo ili wafanye maamuzi sahihi kwa wakati sahihi.

"Ili kukabiliana na tatizo la unyanyapaa, tunatoa wito kwa Waziri wa Afya pamoja na wataalamu wake wawe na programu maalum kwenye runinga kuelezea hatari au madhara ya unyanyapaa ambao unaweza kusababisha vifo zaidi," alisema Canon Matonya.

Vile vile, alisema kwa upande wa wao kama viongozi wa makanisa wataendelea kuelimisha watu kuhusu corona na madhara ya unyanyapaa.

"Watumishi, watendaji katika sekta ya afya wana hali ngumu na ya hatari kwa maana ya kuwa na upungufu wa vifaa tiba ikiwamo vifaa vya kujikinga wenyewe wasipate maambukuzi... tunatoa wito kwa watendaji wa serikali, na tuwashauri kuwa kipaumbele namba moja cha fedha za michango zinazotolewa ili kusaidia na kuwatunza watumishi wa sekta ya afya," alisema.

Pia alisema kuwa jumuiya hiyo imekubaliana kwa pamoja watoto wasiende kanisani na familia zao ziweke utaratibu wa kuwafanyia ibada wakiwa nyumbani.

"Lakini vifaa vinavyotumika katika ibada ikiwamo magitaa, vipaza sauti, meza, viti na vifaa vingine vikavyotumika vifanyiwe usafi wa dawa ya kuvitakasa kabla ya kuanza kutumika," alieleza na kuongeza:

"Na watumishi waache tabia ya kuwaombea wagonjwa kwa kuwagusa na mikono yao wakati huu wa mlipuko wa corona, bali wawanyooshee mikono tu inatosha."




Dereva wa bajaji ambaye jina lake halikupatikana, akiwafungulia mlango wateja wake kandokando ya Barabara ya Nyerere jijini Dodoma jana. Siku hizi kazi zote zinafanywa na makundi ya jinsia zote. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Kuingia ofisi za Sido kwa barakoa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) Mkoa wa Dodoma, limesema kuanzia sasa wateja wake wote watakaofuata huduma kwenye ofisi hiyo, wanatakiwa kuvaa barakoa ili kujikinga na ugonjwa wa homa ya mapafu (COVID-19).

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Sido Mkoa wa Dodoma, Sempeho Manongi, alisema kila mtu anapaswa kuvaa barakoa ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

"Ili kupunguza msongamano Sido inawahimiza wateja na wadau wengine kutumia njia mbadala ya mawasiliano ya simu ili kupata baadhi ya huduma kwa njia ya mtandao na taarifa mbalimbali," alisema Manongi.

Alisema wageni wote watatakiwa kuzingatia maelekezo ya kujikinga na kuwakinga wengine kama inavyoelekezwa na Wizara ya Afya mara kwa mara, ikiwamo kunawa mikono na kupata vitakasa mikono (sanitizer) wakati wa kuingia na kutoka kwenye ofisi hizo.

Alisema shirika hilo litaendelea kuzingatia tahadhari dhidi ya ugonjwa huo bila kuathiri utendaji wa kazi na kuwahudumia wateja.

Mbali na hilo, Manongi aliwataka wajasiriamali kuendelea kufanya kazi zao kwa umakini ili kujikwamua na maisha pamoja na kutangaza biashara zao.

Kwa mujibu wa Manongi, lengo ni wajasiriamali kusonga mbele na sio kukata tamaa kutokana na ugonjwa wa corona.

Hata hivyo, alisema kinachotakiwa hivi sasa ni watu kuchukua tahadhari na kufuata maelekezo ya wataalamu kwenye biashara zao.

"Hakuna sababu ya kubweteka, kinachotakiwa ni kupambana kuhakikisha tunashinda," alisema Manongi.

Aliwataka wajasiriamali wote wafanye kazi ikiwamo kusaidia kutengeneza vitakasa mikono, sabuni pamoja na barakoa ambazo zinahitajika kuvaliwa kipindi hiki cha corona.

Alieleza kuwa matumaini yake ni kuona ujasiriamali unasonga mbele zaidi na watu wanajikwamua kiuchumi kulingana na fursa zilizopo.

# Chawata yaomba wenye ulemavu kukumbukwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI na wadau nchini wamekumbushwa kuwatazama watu wenye ulemavu kwa kuwatengenezea mazingira rafiki na kuwapatia vifaa vya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ulemavu (Chawata), Mkoa wa Mbeya, Jimmy Ambilikile, alisema bado mazingira na miundombinu ya kujikinga na ugonjwa wa Covid-19 imewekezwa zaidi kwa watu walio na ukamilifu wa viungo na kuwaacha katika wakati mgumu wenye ulemavu.

Ambilikile alisema kati ya maeneo yaliyosahaulika kwao ni kutengenezewa miundombinu ya kujikinga na corona ikiwamo vifaa vya kunawia mikono.

"Yako baadhi ya maeneo mwenye ulemavu anapofika analazimishwa kunawa mikono yake kabla ya kupewa huduma jambo ambalo ni sahihi, lakini changamoto inayokuja ni pale chombo cha kunawia kinapokuwa kikwazo maana kilivyotengenezwa sio rafiki kwake," alisema Ambilikile.

**Yako baadhi ya maeneo mwenye ulemavu anapofika analazimishwa kunawa mikono yake kabla ya kupewa huduma jambo ambalo ni sahihi, lakini changamoto inayokuja ni pale chombo cha kunawia kinapokuwa kikwazo maana kilivyotengenezwa sio rafiki kwake**

Alilizungumzia kundi la wenye uoni hafifu wanaotumia fimbo alisema wanaweza kuwa kwenye hatari kubwa ya kupata maambukizo kutokana na vifaa vya kunawia.

Kadhalika mwenyekiti huyo alisema bado kuna changamoto kwa wenye ulemavu wanaojishughulisha na ujasiriamali kwa kuwa utekelezaji wa kuhakikisha maeneo yao yanakuwa na vitakasa mikono ikiwamo maji yanayotiririka ni mgumu kutokana na kutokuwa na uwezo wa kubeba maji kutoka yanakopatikana hadi maeneo ya shughuli zao.



Baadhi ya wajasiriamali wanaouza matunda jijini Mbeya, wakiwa wamepumzika katika moja ya vyumba vya biashara vinavyozunguka uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Miti 200 yapandwa kukabiliana ukame

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

JUMLA ya miti 200 ya aina mbalimbali imepandwa kwenye Kituo cha Afya cha Kapunga, Kata ya Itamboleo, wilayani Mbarali, mkoani hapa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ikiwamo ukame.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo juzi, Michael Semindu, aliongoza upandaji miti hiyo na kusema pia itapendezesha mandhari kuzunguka kituo hicho cha afya.

Alisema upandaji miti wilayani humo ni endelevu kwa sababu ya jiografia ya eneo hilo kuwa na ukame hivyo watakuwa wanaotesha miti mara kwa mara.

Baada ya kukamilisha upandaji miti katika kituo hicho, Semindu aliwataka wakazi wote kuhakikisha wanapanda miti katika maeneo ya wazi pia katika makazi yao kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kuondokana na hali ya ukame.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya hiyo, Kivuma Msangi, aliwaomba watendaji wote wa kata na vijiji kuwahamasisha wananchi katika maeneo yao kupanda miti ya aina tofauti kwa sababu itawasaidia kwa mambo mbalimbali.

Alisema wilaya itaendelea na jukumu la kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya kutolea huduma za kijamii, pia wananchi waendelee kufanya hivyo kwenye maeneo wanayoyazunguka.

Diwani wa Viti Maalum kutoka Igurusi, Lucy Ngondo, aliiomba halmashauri kuzalisha kwa wingi miche ya miti ili kuwagawia bure wananchi wengine ambao hawana uwezo wa kumudu gharama kununua.

Alisema baadhi ya wakazi hususani wazee wanaomiliki miji hawana uwezo wa kumudu gharama za kununua miche ya miti, alishauri viongozi kuandaa utaratibu maalum kuwagawia ili nao waendane na kasi ya upandaji miti.

# Shirika latoa msaada kujikinga virusi corona

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

SHIRIKA lisilokuwa la kiserikali la The Olive Branch linalofanya shughuli zake za kijamii katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, limetoa msaada wa barakao 200, vidonge vya klorokwini 200, glovu 500 na vitakasa mikono lita 20 kwa uongozi wa wilaya ili kusaidia mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covid-19.

Akikabidhi msaada huo jana, Mratibu wa Shirika hilo, Daud Silingi, alisema una lengo la kuunga mkono juhudi za kukabiliana na maambukizo ya virusi vya corona na jumla ya Sh. 931,000 zimetumika.

Alisema waliguswa kutoa msaada huo baada ya kubaini kuna uhitaji mkubwa wa vifaa katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo na kuongeza kuwa baadhi ya wananchi hutumia vifaa ambavyo haviwezi kujikinga na maambukizo ya corona.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya, Reuben Mfune, amelishukuru shirika hilo kwa kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo hatari na kuwaomba kuendelea kusaidia kwa sababu mahitaji bado ni makubwa.

Alisema vifaa vilivyotolewa vitagawiwa kwenye maeneo muhimu ya kutolea huduma hususani kwenye vituo vya afya na zanahati ambazo kwa sasa zina uhitaji mkubwa wa barakoa, ndoo za maji, glovu na vitakasa mikono.

Alisema eneo la huduma za afya litapewa kipaumbele kwa sababu linapokea wagonjwa wa kila aina na wanahitaji vifaa vingi ili kuwahudumia wananchi kwa tahadhari kubwa na usalama.

Aliwataka wadau wengine wa maendeleo kuiga mfano uliotolewa na Shirika la The Olive Branch, kujitokeza ili kusaidia juhudi za kupambana na virusi vya corona ambavyo ni tishio nchini na mahitaji ya vitendea kazi na vifaa vya kujilinda bado ni makubwa.

"Ninalishukuru shirika hili kwa kuguswa na kuamua kutoa vifaa hivi ili kusaidia juhudi za kupambana pamoja na kujikinga na ugonjwa wa Covid -19, vitasaidia sana kwenye maeneo ya kutolea huduma za afya ambako bado kuna uhitaji," alisema Mfune.

Pia alisema bado wilaya yake ina mahitaji makubwa ya vifaa vya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona na kuwaomba wadau wengine kujitokeza kusaidia mapambano hayo.





# Maimamu watakiwa kuchukua hadhari corona nyumba za ibada

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BARAZA la Maulama la Zanzibar limewataka Maimamu kuchukua tahadhari za kujiepusha na ugonjwa wa corona katika nyumba za ibada na kuacha kuzusha malumbano ambayo baadhi yake yamepelekea kufungwa kwa misikiti Zanzibar.

Hayo yalisemwa na Mjumbe wa Baraza la Maulama la Zanzibar, Sheikhe Thabit Nouman Jongo, ambaye alisema ibada ya sala haiwezi kuwa batili kwa Waislamu kusali kwa kuweka nafasi ya mita moja na nusu katika misikiti.

Alisema suala la kufanya ibada na kuweka nafasi kati ya mtu na mtu limekuja kwa njia ya dharura kwa ajili ya kuepusha maafa.

''Sala haiwezi kuwa batili kwa sababu watu wamesali kwa kuweka nafasi kati ya mtu mmoja na mwingine...huo ni utaratibu ambao umekuja kwa njia ya dharura kwa ajili ya kuepusha maradhi," alisema.

Mwalimu Mkuu wa Chuo cha Kiislamu Zanzibar, Sheikhe Muhidin Siasa, aliwataka Maimamu kuacha kulumbana katika jambo ambalo lipo wazi ambalo limekuja kwa njia ya dharura kuepusha maafa.

Alisema katika enzi za mitume mbalimbali yalikuwapo maradhi ya kuambukiza na kupelekea waumini kufanya ibada majumbani kwa lengo la kuepusha maafa.

Alisema zipo baadhi ya nchi za Kiislamu zimechukua maamuzi magumu ambayo hayajawahi kufanywa, na kutoa mfano wa Sauda Arabia ambayo imesitisha ibada ya Umra, ambayo hiki ni kipindi chake kwa waumini wa dini ya Kiislamu kuzuru Macca katika Alkaaba.

"Natoa mfano mzuri wa Sauda Arabia imefuta ibada ya Umra katika mji mtakatifu wa Macca kwa hofu na tahadhari ya ugonjwa wa corona kwa kuepusha kuzuka kwa maambukizi zaidi," alisema.

Mjumbe wa Baraza la Maulama la Zanzibar kutoka Mkoa wa Magharibi Unguja, Suwedi Ali Suwedi, alisema suala la kuweka masafa katika kufanya ibada lisiwagawe Waislamu na kupelekea kufunga kwa misikiti.

''Wapo Maimamu wameifunga misikiti na kuzuia Waislamu kushindwa kufanya ibada kwa sababu tu ya kubishana kuhusu kuweka nafasi kati ya mtu mmoja na mwingine kwa lengo la kuepuka maambukizi ya corona," alisema.

Baraza la Maulama la Zanzibar likiongozwa na Mufti wa Zanzibar limetoa masharti ya kufanya ibada katika kipindi hiki, na kuwataka Waislamu kuweka nafasi mita moja na nusu kati ya mtu na mtu ikiwa tahadhari ya maambukizi ya corona, tamko ambalo limekosolewa na baadhi ya Maimamu na kusababisha kufungwa kwa baadhi ya misikiti.

Baadhi ya misikiti iliyofungwa ni wa Mchangani uliopo eneo la biashara la Darajani na baadhi nje ya mji wa Unguja.



Wafanyabiashara wa viazi vitamu wakisubiri wateja katika eneo la Chanika, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam jana. Viazi hutumika katika maandalizi ya futari hasa katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

## Marufuku kuingia Kusini Pemba bila kuvaa barakoa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed Suleiman, amepiga marufuku wananchi kuingia katika Mkoa huo wenye harakati nyingi ikiwamo bandari kuu bila ya kuvaa barakoa.

Suleiman alitoa agizo hilo wakati akizungumza na viongozi wa mkoa wakiwamo wakuu wa wilaya na masheha ikiwa ni sehemu ya mikakati ya tahadhari ya kuepuka maambukizi ya corona.

Alisema Mkoa wa Kusini una harakati nyingi za watu ikiwamo bandari kuu ya Mkoani, hivyo kuna haja ya tahadhari kupambana na ugonjwa huo.

Alieleza baadhi ya watu wanakaidi amri na maagizo yanayotolewa na serikali, ikiwamo kuendelea kufanya mikusanyiko bila ya sababu za msingi.

Alisema katika eneo la Bandari ya Mkoani ambayo hupokea na kuingiza meli za abiria zinazotoka Unguja na Tanga, tahadhari zimechukuliwa ikiwamo kupima wananchi toto la mwili pamoja na kuweka vifaa vya kinga.

''Serikali ya Mkoa wa Kusini Pemba tumepiga marufuku mtu yeyote kuingia katika mkoa huu bila ya kuvaa barakoa ikiwa ni sehemu ya tahadhari ya kujikinga na ugonjwa wa corona," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mkoani, Ali Issa, aliwataka masheha kujipanga vizuri katika shehia zao kuhakikisha kila mtu anavaa barakoa ikiwa ni hatua ya kujikinga na corona.

Aidha, aliwataka masheha kuendelea kufanya ukaguzi wa watu ambao wanaingia katika maeneo yao bila ya kuhakikiwa, ikiwamo kukaa siku 14 kwa ajili ya tahadhari ya corona.

''Tumewapa maagizo masheha wote kuhakikisha kwamba wanachukuwa tahadhari ya kujikinga na corona ikiwamo kuorodhesha watu wote wanaoingia katika maeneo yao," alisema.

# Sheha aasa watoto ngoma za vigodoro

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHEHA wa Shehia ya Kibweni, Subira Haji Yahya, amewataka wazazi na walezi kutowaogopa watoto wao na kuhakikisha wanawakataza vitendo viovu ikiwamo ngoma za vigodoro.

Akizungumza na Nipashe, alisema baadhi ya wazazi katika shehia yake wamekuwa wakiwaogopa watoto wao na kushindwa kuwakataza mambo maovu.

Alisema baadhi ya wasichana wamejikita katika vitendo viovu, ikiwamo kushiriki katika ngoma za vigodoro na kudharau masomo.

Alieleza kuwa wasichana hao bado ni wanafunzi na wengine wameshatoroka shule, jambo ambalo ni hatari kwao.

"Kwa kweli watoto hawataki kuwasikiliza wazazi wao, wameunda kikundi wanacheza ngoma ya kigodoro, tena baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwakatia sare na kuwanunulia vijora," alisema.

Alieleza kuwa alishawaita wazazi na watoto wanaojihusisha na vitendo hivyo viovu, ikiwamo kushiriki katika mapenzi wakiwa na umri mdogo.

Alieleza kuwa licha ya elimu aliyoitoa kwa wazazi na watoto hao, lakini bado haijafanikiwa kwa sababu watoto hao wanaendelea kufanya vitendo viovu.

"Hivi karibuni nililetewa kesi kati ya hao watoto, ambapo mmoja ana miaka 15 analalamikiwa kuchukua mume wa mtu, kwa kweli watoto wetu wana mitihani," alisema.

Alizitaka taasisi za wanaharakati wa kutetea haki za wanawake na watoto kufika katika shehia hiyo kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii ili watoto waweze kuepukana na vitendo vya udhalilishaji.

Naye Asha Ali (mzazi), alisema wanajitahidi kuwaeleza watoto wao, lakini hawataki kuwasikiliza.

"Mimi husema na mtoto wangu mpaka wakati mwingine nalia kwa hasira kutokana na mwenendo anaoenda mtoto wangu sio mzuri, lakini hataki kunisikiliza hivi sasa shule katoroka hataki tena kusoma sijui anategemea nini," alisema.

Mratibu wa wanawake na watoto wa shehia hiyo, Hidaya Muhamed, alisema wanajitahidi kutoa elimu kwa jamii hasa watoto wa kike ili kufuatilia masomo na kuachana na mambo yasiyowahusu.

Aidha, aliwataka wazazi na walezi kuwachunga watoto wao wakiwa wadogo kwani wanapofikia umri wa kuvunja ungo, inakua vigumu kuwadhibiti.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa)-Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema watoto wanahitaji uangalizi wa karibu wa wazazi na walezi kwa sababu katika jamii wanakutana na vishawishi vingi, ambapo mara moja hushawishika na hatimaye kufanyiwa udhalilishaji.

Aliitaka jamii kuwa na malezi ya pamoja kwa watoto wote na pale mzazi anapomkataza jambo mtoto ambaye sio wake amsikilize, badala ya kuona anamwonea.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

**WANAHITAJIKA WAFANYAKAZI**
Wanahitajika wasichana wa kuuza Duka na wa kazi za ndani , Wanahitajika haraka sana. Piga Simu namba : **0715 431528 au 0784 431528**

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTELEWA NA VYETI



115729102

**Edward Fidel** amepotelewa na cheti cha chuo kikuu cha Dodoma kilichotolewa mwaka 2019 na cheti cha matokeo ya elimu ya chuo kikuu cha Dodoma cha mwaka 2019. vyeti hivyo viliibiwa vikiwa nyumbani kwao.

Kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa polisi au awasiliane naye kwa namba **0758-632226.** Ametoa taarifa polisi na kupewa RB na. **Kag/buk/rb/218518/2020 na Kag/buk/rb/142573/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



215729302

**Anthony Kenneth Maneno** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3674/0060 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013, katika shule ya Sekondari St. Joseph's Millenium. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/MAG/RB/296321/2020**

**JAHMURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**
**WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LA MADAI NA. 55/2020**

**MDAI.......................................... CLARA EPHRAHIM**

**DHIDI YA**

**MDAIWA.....................................CLEMENT ROBERT**

**POPOTE PALE TANZANIA BARA NA VISIWANI**

**AMRI**
Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakama mnamo tarehe 7-5-2020 saa 2:30 Asubuhi bila kukosa. Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo, na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo Alhamisi tarehe 23 mwezi April 2020

## KUPOTEA KWA KADI YA TRACTOR SONALIKAP

**MARTIN ZAKARIA KIBAJA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Tractor yenye namba za usajili **T 136 AYJ** aina ya **SONALIKA TRACTOR**. Engine: **4100FL72E119732.**Chassis: **FZBDY1191973.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MUH/RB/4146/2019.**

215729802

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
04/05/2020

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMANNE** tarehe **05/05/2020** kampuni ya **AGURE TRANSPORT LIMITED.** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa. Kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **RUSUMO kupitia VIGWAZA**

   Gari hilo lina namba za usajili: **T702 DRC/T497 DQV**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.2** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.0** |

   Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;101/2020**

**Ombi la PHILEMON FESTO MSECHU Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu TELESIA MOHAMED MASENGO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 23/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/04/2020.

HAKIMU

115729702

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KANDA YA MWANZA**

**SHAURI LA MAOMBI NAMBA 10 YA MWAKA 2020**

**RECHO JOSHUA...................................MDAI**

**DHIDI YA**
**MEDA JOSEPH.....................................MDAIWA**

**KWA; MEDA JOSEPH**

**KUITWA SHAURINI**

UNA ARIFIWA KUHUDHULIA HAPA MAHAKAMANI 14/05/2020, KUJA KUSIKILIZA SHAURI LA MADAI YALIYOFUNGULIWA NA MDAI DHIDI YENU.

UNATAHADHARISHWA KUWA ENDAPO HAUTOFIKA SIKU HIYO SHAURI LITASIKILIZWA UPANDE MMOJA DHIDI YENU NA KUTOLEWA MAAMUZI.

HATI HII IMETOLEWA KWA MKONO WANGU NA CHAPA YA MAHAKAMA LEO HII TAREHE 22/04/2020.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA

215729202

**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.28 2020**

**In the matter of the Estate of the LATE ROBERT KWALU NDAKI of Nkuhungu within Dodoma city**

**And**

**In the matter of the Application for letters of Probate and Administration of estate by NDAKI ARNOLD NDAKI**

**GENERAL CITATION**
***(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 163)***

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 15/05/2020.

Dated at Dodoma this 04th day of March 2020

Petitioner
Presented for filling this 08/04/2020

RESIDENT MAGISTRATE

DRAWN AND FILED BY:
MWAIPOPO AND ASSOCIATES ADVOCATES
P. O. BOX 1723, DODOMA

COPY TO BE SERVED TO:
THE HEIRS

215729902

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**EAST AFRICAN COMMUNITY SECRETARIAT** INATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO TCDM1 EAC ENGINE NO **27892830173376** CHASSIS NO **WDC166873A368659** STATION WAGON YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI **ARU/ARU/RB/352319/2020.**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Benki yasamehe wateja waliokopa

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

BENKI ya Absa ya Afrika Kusini imekubali kuwasamehe kwa muda ulipaji wa madeni ya mamilioni ya dola,wateja wao waliokopa.

Hatua hiyo imetokana na sekta hiyo kusema watu milioni 1.2 wametuma maombi ya kutaka msaada.

**Uchumi wa Taifa hilo tayari umetumbukia katika mdororo tokea mwishoni mwa mwaka 2019.**

Athari za kufungwa kwa shughuli za kijamii nchini Afrika Kusini nchi yenye watu milioni 58 kutokana na uwapo wa ugonjwa wa corona inatarajiwa kuwa kubwa.

Uchumi wa Taifa hilo tayari umetumbukia katika mdororo tokea mwishoni mwa mwaka 2019 na kiwango rasmi cha wasiokuwa na ajira kikifikia asilimia 30.

Absa ambayo ni moja kati ya taasisi nne kubwa za ukopeshaji imesema zaidi ya wateja 376,000 kati ya wateja wake wameomba msaada.

Imesema imekubali kutoa msaada wa randi bilioni 5.8 kutowa afueni ya kurudisha mkopo au kupunguza madeni hayo kwa awamu katika kipindi cha miezi mitatu. **DW**



Wananchi katika Jiji la Rome, Italy, wakiwa mitaani baada ya kuondolewa kwa katazo la watu kuzurura. **PICHA: REUTERS**

## Corona kuahirisha uchaguzi Poland

**WARSAW,** Poland

WAZIRI Mkuu wa Poland, Jacek Sasin, amesema itakuwa vigumu kuandaa uchaguzi wa rais nchini humo katika tarehe iliyopangwa ya Mei 10.

Amesema kwamba kuna uwezekano uchaguzi huo ukaahirishwa hadi Mei 17 au Mei 23. Chama tawala cha Haki na Sheria cha PiS, kinajaribu kufanya liwezekanalo ili uchaguzi huo ufanyike licha ya mgogoro wa kiafya uliyosababishwa na ugonjwa wa virusi vya corona kwa kupendekeza marekebisho ya sheria za uchaguzi ambao utawezesha upigaji kura unafanyika kupitia njia ya posta.

Lakini sheria inayoruhusu kura hiyo ya posta bado haijakubaliwa na bunge la seneti, uchaguzi wa awali unaonyesha kwamba chini ya asilimia 30 ya raia wa Poland wako tayari kupiga kura ikiwa uchaguzi utafanyika Mei 10 kama ilivyopangwa.

"Mei 10 itakuwa vigumu, Ikiwa imesalia wiki moja kabla ya uchaguzi, raia wa Poland bado hawajui kama watapiga kura. Upinzani na bunge la seneti ndiyo wanahusika na hali hii," alisema Sasin kwenye redio binafsi ya Zet.

Upinzani nchini humo, makundi ya haki za binadamu na Umoja wa Ulaya (EU) wamebaini kwamba, kufanyika kwa uchaguzi katika mazingira yaliyowekwa na serikali hakutakuwa na uwazi na kutadhoofisha demokrasia nchini humo. **RFI**

# Dawa ya corona yaanza kujaribiwa

**LONDON,** Uingereza

NCHI ya Uingereza imeanza kufanya majaribio ya dawa ya kutibu ugongwa wa virusi ya corona.

Kaye Flitney ni mmoja wa watu waliojitolea kujumuishwa katika majaribio ya dawa mpya ya kukabiliana na virusi vya corona. Kaye, (67), ambaye kwa sasa yupo kitandani, anasumbuliwa na kikohozi.

Alisema kwa mara ya kwanza alipogundua ana virusi vya corona fikra yake ya kwanza ilikuwa siyo kuangalia afya yake.

"Nilitishika kwa sababu mume wangu ana tatizo la moyo. Itamuua," alisema Kaye.

Mwanamke huyo ambaye alipelekwa hospitalini kutokana na tatizo la kupumua, alisema kwamba matumizi wa dawa hiyo haijamsababishia tatizo lolote.

Dawa hiyo iliyotengenezwa na wanasayansi wa Uingereza kutibu ugonjwa wa virusi vya corona inafanyiwa majaribio katika Chuo Kikuu cha Southampton.

Ikiwa imetenegenezwa na kampuni ya Synairgen , inatumia protini kwa jina interferon beta, ambayo hutoka katika mwili wa binadamu anapopata maambukizo ya virusi. Matokeo ya majaribio hayo yanatarajiwa kutolewa mwishoni mwa mwezi Juni. Kwa sasa kuna dawa chache zinazoweza kutibu virusi hivyo huku madaktari wakitegemea kinga ya wagonjwa wao.

Interferon beta ni dawa inayolinda mwili wa binadamu dhidi ya virusi, ikionya dhidi ya shambulio la virusi , kulingana na Richard Marsden. Ofisa Mkuu Mtendaji wa kampuni ya Synairgen iliopo makao yake mjini Southampton alisema kwamba virusi vya corona hujaribu kukabiliana na uzalishaji wake kama mpango wa kutaka kukwepa mfumo wa kinga mwilini.

Dawa hiyo ina muundo maalum wa interferon beta inayowekwa moja kwa moja kwenye njia za hewa wakati zilizopo na virusi, kwa matumaini kwamba kipimo cha protini moja kwa moja kitatoa majibu ya kupambana na virusi hata miongoni mwa wagonjwa ambao kinga zao tayari ni dhaifu.

Interferon beta hutumika sana kutibu ugonjwa wa kupooza. Synairgen tayari imethibitisha kwamba maandalizi yake yanaweza kuimarisha kinga katika mapafu ya mgonjwa mwenye pumu na magonjwa sugu ya mapafu.

Alisema bado haifahamika iwapo inaweza kukabiliana na ugonjwa wa virusi vya corona baada ya kufanyiwa majaribio kadhaa miongoni mwa binadamu. **BBC**

## Walioambukizwa corona duniani wafikia milioni 3.5

**PARIS,** Ufaransa

MAAMBUKIZO ya ugonjwa wa virusi vya corona duniani yamefikia milioni 3.5, wakati idadi ya vifo vilivyotokana na ugonjwa huo vikiongezeka na kufikia 245,000.

Viwango vya maambukizo mapya na vifo vimepungua ikilinganishwa na mwezi uliopita, kulingana na ripoti ya Shirika la Habari la Reuters.

Matukio mengi yaliyothibitishwa katika siku za hivi karibuni yaliripotiwa katika ukanda wa Amerika ya Kaskazini na nchi za Ulaya, ingawa idadi ya kila siku ya maambukizo mapya inaongezeka katika ukanda wa Amerika ya Kusini, Afrika na Urusi.

Duniani kote, visa vipya 84,004 viligunduliwa ndani ya masaa 24 yaliyopita, Shirika la Habari la Reuters limebaini, huku likijikita katika takwimu rasmi zilizotolewa na kila idadi ambayo inafanya jumla ya visa duniani kote kufikia zaidi ya milioni 3.5.

Vifo vinavyotokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona vimefikia 245,992.Kifo cha kwanza cha mtu aliyefariki wa ugonjwa wa virusi vya corona kiliripotiwa Januari 10 katika nchi ya China huko Wuhan, jiji ambalo virusi hivyo vilianzia mwezi Desemba mwaka jana.

Kiwango cha kila siku cha maambukizo ya virusi ulimwenguni kilisalia kati ya asilimia mbili na tatu wiki iliyopita, dhidi ya asilimia 13 katikati ya mwezi Machi, na kusababisha nchi nyingi kuanza kulegeza masharti ya watu kutotembea ili kuendeleza shughuli mbalimbali, wakati mgogoro wa kiafya umezorotesha uchumi wa dunia.**RFI**

# SANE HANA THAMANI YA EURO MIL. 100 - KOCHA




**MUNICH,** Ujerumani

JUPP Heynckes anahisi mshambuliaji wa Manchester City, Leroy Sane bado hajawa "mchezaji wa daraja la juu" na anaamini winga huyo anayewaniwa na Bayern Munich hana thamani ya euro milioni 100.

Sane mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akihusishwa sana na kutakiwa Bayern kabla ya kuumia goti Agosti mwaka jana.

Miamba hao wa soka la Ujerumani wameripotiwa kumuwania Sane, lakini Heynckes - ambaye alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na mataji manne ya Bundesliga akiwa kocha wa Bayern - amesema mshambuliaji huyo hayupo miongoni mwa wachezaji bora duniani.


"Alikuwa kwenye muelekeo mzuri kabla hajaumia vibaya. Kwa upande wangu, bado hajawa mchezaji wa daraja la juu,"alisema akiiambia Welt am Sonntag.

"Nafikiri kwa sasa ni mchezaji ambaye 'anavuka barabara'. Ataendelea kujiimarisha kwa bidii zaidi, au aendelee kuwa mchezaji mwenye kipaji cha kawaida?"

Bayern imeripotiwa kujiandaa kulipa angalau euro milioni 100 kwa ajili ya Sane, ingawa pengine mambo yanaweza kubadilika kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Pamoja na hilo, Heynckes hafikirii kama Sane mwenye umri wa miaka 21, raia wa Ujerumani anaweza kuwa na thamani na kiwango hicho cha fedha.

# *Alcantara atamani kuzeekea Bayern Munich*



**MUNICH,** Ujerumani

NYOTA wa Bayern Munich, Thiago Alcantara, amesema "itamfurahisha" kumalizia soka lake kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, huku akimsifia mchezaji mwenzake anayecheza kwa mkopo hapo, Philippe Coutinho.

Thiago alijiunga na Bayern akitokea Barcelona mwaka 2013, na raia huyo wa Hispania mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2020-21, huku kocha Hansi Flick akiwa na matumaini ya kuendelea na kiungo huyo.

Tangu atue Munich, Thiago ameshinda mataji sita ya Bundesliga na sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, yupo tayari kustaafia soka kwa miamba hao wa Bavaria.

"Hilo ni swali gumu. Mambo mengi yanatakiwa kuja pamoja," alisema Thiago akiliambia gazeti la Catalunya, La Vanguardia wakati alipoulizwa kama anajiona kwamba atamalizia soka hapo Bayern. "Ningependa kubakia hapa.

"Pengine ghafla klabu itaangalia mchezaji mpya wa nafasi yangu. Lakini litakuwa jambo la kufurahisha kumalizia soka langu kwenye klabu hii."

Thiago pia aliulizwa kuhusu Coutinho, ambaye alijiunga na Bayern kwa mkopo wa muda mrefu kutoka kwa mabingwa wa LaLiga, Barca mwanzoni mwa msimu huu.

Coutinho alikuwa na wakati mgumu wa kujiimarisha yeye mwenyewe hapo Bayern, pia alishindwa kuwa kwenye kiwango cha kuvutia tangu alipoondoka kule Liverpool na kutua Barca mwaka 2018.

"Namjua vizuri sana, yuko poa," alisema Thiago. "Nimemuona akicheza tangu akiwa na umri wa miaka 12. Nimecheza dhidi yake nchini Brazil na nampenda."

# Chelsea sasa kwa Ter Stegen

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea imeonyesha nia ya kuwania kumsajili golikipa wa Barcelona, Marc-Andre Ter Stegen, huku kukiwa na ripoti kuwa kocha Frank Lampard yuko tayari kumuuza Kepa Arrizabalaga kwenda Real Madrid.

Licha ya kuhusishwa na Gianluigi Donnarumma wa AC Milan na Andre Onana wa Ajax, pia Chelsea inatajwa kuisaka saini ya Ter Stegen anayedaiwa kuwa mbioni kuondoka huko Nou Camp baada ya kudaiwa kugombana na nahodha wake, Lionel Messi.

Inasemekana Messi amewataka viongozi wa Barcelona kumuuza Ter Stegen, huku pia akiwataka viongozi wa timu hiyo kumfuata Neymar mwenye thamani ya pauni milioni 198.

Wakati Chelsea ikiwekeza nguvu zake kwenye kusaka saini ya Ter Stegen inadaiwa kuwa Real Madrid imeanza harakati za kuisaka saini ya Kepa ambaye anaonekana kupoteza imani ya Lampard, na huenda akaondoka.



## HABARI MICHEZO

# Martinez ashauriwa kubakia Inter

**MILAN,** Italia

BORJA Valero amemshauri mchezaji mwenzake wa Inter Milan, Lautaro Martinez, kupuuzia mpango wa kutakiwa na Barcelona na abakia hapo kwenye dimba la San Siro, wakati akimsifia mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina.

Martinez amekuwa akipamba vyombo vya habari msimu huu akihusishwa na mpango wa kutakiwa kwa muda mrefu na Barcelona. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amefunga mabao 16 msimu huu katika mashindano yote aliyowachezea Nerazzurri hao, akiwa pamoja na Romelu Lukaku.

Baada ya kufunga mabao tisa kwa msimu wote wa 2018-19, Valero anaamini Martinez ni mchezaji wa Inter aliyeimarika zaidi. Na kiungo huyo wa zamani wa Fiorentina anamtaka Martinez kubakia hapo kwenye Jiji la Milan.

"Kutoka mwaka hadi mwaka, yeye ndio mchezaji aliyeimarika zaidi," alisema Valero akiliambia gazeti la Gazzetta dello Sport.

"Kwa nyongeza ni mfungaji mzuri na anafanya kazi ya kuridhisha sana kwa timu nzima."

Alipoulizwa kwa nini Martinez anatakiwa abakie Inter kuliko kwenda Barcelona, Valero alisema: "Hapa tuna mradi muhimu sana. Ipo wazi kwa kila mtu. Ili mradi wetu ukamilike, tunamhitaji abakie na sisi."






# RASHFORD AFANANISHWA NA MBAPPE MBIO BALLON D'OR

**MANCHESTER,** England

MARCUS Rashford anaweza kufikia daraja la Kylian Mbappe na kwenda kushinda Ballon d'Or, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa Manchester United, Matteo Darmian.

Rashford amefurahia zaidi msimu wa 2019-20 kwa kufunga mabao, akiwa ametikisa nyavu mara 19 katika mashindano yote kwa 'Mashetani Wekundu' hao, licha ya kuwa nje ya uwanja tangu Januari kutokana na kuumia mgongo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alichomoza mwanzoni mwa mwaka 2016 chini ya kocha, Louis van Gaal, akifunga mara mbili katika mechi ya Ligi ya Europa na Ligi Kuu ya England yakiwa ndio mabao yake ya kwanza tangu alipopandishwa kutoka akademi ya vijana.

Hata hivyo, Darmian, hashangazwi na maendeleo mazuri ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22.

"Bado namkumbuka Marcus Rashford katika mazoezi yake ya kwanza kwa timu ya wakubwa, ni kama jana tu. Haraka nashangaa, 'wow, kumbe ni mchezaji wa aina yake'," alisema akiliambia gazeti la The Guardian.

Mlinzi huyo wa Italia, ambaye alirudi nyumbani kwao Septemba mwaka jana na kusajiliwa pale Parma, anahisi mchezaji huyo wa kimataifa wa England bado anaweza kuwa bora zaidi.

Darmian anahisi Rashford ana nafasi kubwa ya kuwa sawa na nyota wa Paris Saint-Germain, Mbappe, na kwamba wawili hao wanaweza kushindana kwa miaka mingi ijayo katika kuwania tuzo binafsi.

"Kama yeye (Rashford) anaendelea kucheza kwa bidii na kujituma nina uhakika anaweza kushinda tuzo ya Ballon d'Or. Nashawishika kabisa kuamini hilo," alisema.

# *Origi amganda Klopp*

**LIVERPOOL,** England

DIVOCK Origi pengine anajiimarisha mwenyewe licha ya kupata nafasi chache za kucheza pale Liverpool na sasa amebainisha anataka kuendelea kucheza chini ya Jurgen Klopp.

Origi alijiimarisha yeye mwenyewe hapo Anfield kama shujaa msimu uliopita kwa mabao yake muhimu, likiwamo la kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Tottenham.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, amefunga mabao zaidi matano katika mashindano yote msimu huu, lakini mafanikio yake yamefichwa na nyota Mohamed Salah, Roberto Firmino na Sadio Mane.

Origi alisaini mkataba wa "muda mrefu" pale Merseyside Julai mwaka 2019, na anaendelea kuonyesha kwamba harudi nyuma.

"Mimi ni mchezaji bora zaidi kuliko mwaka jana," alisema mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 25, akiliambia gazeti la Het Laatste Nieuws. "Klopp amenipa nafasi ya kujiimarisha mimi mwenyewe. Mara zote namsikiliza na nataka kuendelea kucheza chini yake.

"Tunazungumza mara kwa mara na nina uhakika nikiwa chini yake nitaimarika zaidi na zaidi."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DYBALA, HIGUAIN KUBAKISHWA JUVE

●●● Pia kumekuwa na majadiliano na wakongwe Chiellini na Buffon kuongezwa mikataba...

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus inapanga kumbakisha Paulo Dybala "kwa muda mrefu inavyowezekana" na Gonzalo Higuain kwa msimu wa 2020-21, huku Giorgio Chiellini na Gianluigi Buffon nao wakijiandaa kuongeza mikataba yao.

Huku Cristiano Ronaldo kwa sasa akiwa ndiye nyota anayeongoza kwenye kikosi hicho cha Bianconeri, washambuliaji wenzake, Dybala na Higuain wamehusishwa kuondoka hapo Turin.

Dybala aliripotiwa kuwaniwa na Manchester United na Tottenham mwaka jana, wakati Higuain akionekana kupanga kuondoka moja kwa moja baada ya kutokuwa na mafanikio kule AC Milan na Chelsea alikokwenda kucheza kwa mkopo.

**Washambuliaji hao wa Argentina kwa ujumla wamefunga mabao 21 kwa Juve kwenye mashindano yote msimu huu, na Mkurugenzi wa Soka, Fabio Paratici anataka kuwabakisha wote wawili.**

Kumekuwa na majadiliano kuhusu kuongezwa mikataba ya wakongwe Chiellini na Buffon – na Paratici ameiambia Sky Sport Italia: "Chiellini na Buffon wapo kwenye nafasi nzuri.

"Kwa upande wa Dybala, nafikiri majadiliano yake yamesimama kwa muda. Lakini malengo yetu ni kumbakisha hapa kwa muda mrefu kadiri inavyowezekana."

Mkataba wa sasa wa Dybala unamalizika mwaka 2022, lakini klabu hiyo imekuwa kwenye mazungumzo ya kumuongezea mkataba mpya kwa muda mrefu msimu huu wa 2019-20.

Wakati huo huo, Higuain mwenye umri wa miaka 32, mkataba wake unamalizika mwisho mwa msimu ujao, na bado Juventus haijaonyesha nia ya kutaka kumuachia mchezaji huyo wa zamani wa Napoli.

## ZISIKUPITE

### MKHITARYAN KUUZWA

KLABU ya Arsenal iko tayari kumuuza kiungo wake wa kati wa Armenian, Henrikh Mkhitaryan msimu huu ili kupata fedha. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, kwa sasa anacheza kwa mkopo kule AS Roma. ***(Mirror)***

### SPURS YAJITOSA KWA RAKITIC

KLABU ya Tottenham Hotspur inaongoza katika kinyang'anyiro cha kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Barcelona na Croatia, Ivan Rakitic mwenye umri wa miaka 32. ***(Mundo Deportivo)***

### INTER YAMTAKA POGBA

INTER Milan inataka kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba, mwenye umri wa miaka 27. ***(Gazzetta dello Sport)***

### PEDRO AWINDWA BETIS, ROMA

MCHAMBULIAJI wa Chelsea na timu ya Taifa ya Hispania, Pedro mwenye umri wa miaka 32, anawindwa na klabu za AS Roma ya Italia na Real Betis ya Hispania. ***(Goal)***

### ANG'ANG'ANIA SPURS

KIUNGO wa Ufaransa, Tanguy Ndombele, mwenye umri wa miaka 23, yuko tayari kubaki kupigania nafasi yake katika timu yake ya Tottenham licha ya kwamba Barcelona imeonyesha nia ya kutaka kumsajili. ***(Mirror)***

### VAZQUEZ AIWAZIA EPL

WINGA wa klabu ya Real Madrid na Hispania, Lucas Vazquez, mwenye umri wa miaka 28, anasema wazo la kucheza katika klabu moja ya England ni jambo linalomfurahisha. ***(Guardian)***

### ARSENAL, CHELSEA VITANI

ARSENAL na Chelsea zote zimeripotiwa kuwania kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Klabu ya Feyenoord raia wa Uturuki, Orkun Kokcu, 19. ***(Express)***

### SEVILLA YAMTAKA BAKAYOKO

KLABU ya Sevilla inammezea mate kiungo wa kati wa Ufaransa, Tiemoue Bakayoko. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, yuko kwa mkopo katika klabu ya Monaco akitoka Chelsea. ***(France Football)***

### UTD KWA NYOTA WA LEIPZIG

KLABU ya Manchester United imewasiliana na mwakilishi wa mchezaji Ibrahima Konate mwenye umri wa miaka 20, anayekipiga kule RB Leipzig kwa ajili ya kutaka kumsajili. ***(Le10 Sport)***

### STAM KUINOA CINCINNATI

MLINZI wa zamani wa Machester United na Uholanzi, Jaap Stam mwenye umri wa miaka 47, amesema amefanya mazungumzo na FC Cincinnati ya kuwa kocha mpya wa timu hiyo. ***(Goal)***

### S'AMPTON YAMULIKA REIMS

KLABU ya Southampton ina matumaini ya kumnasa mlinzi wa timu ya Reims na Ufaransa, Axel Disasi mwenye umri wa miaka 22. ***(Mail)***

## Kagera Sugar yapania 5-bora

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

LICHA ya kushika nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, Kocha Msaidizi wa Kagera Sugar ya mkoani Kagera, Ally Jangalu, amesema malengo yao ni kumaliza katika nafasi ya tano msimu huu.

Tayari Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi (TPLB), Almas Kasongo, ameeleza ligi hiyo inatarajiwa kurejea Juni mwanzoni endapo watapata baraka zote kutoka kwa serikali ambayo Machi 17, mwaka huu ilisitisha shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19).

Na wakati inasimama Kagera Sugar ilikuwa katika nafasi ya nane ikiwa na alama 41 baada ya kushuka dimbani mara 29, lakini Jangalu amesema licha ya kuwamo kwa changamoto mbalimbali watakahikisha wanamaliza nafasi tano za juu.

"Lengo letu ni kutaka kushika nafasi ya tano mwaka huu, mbali na kwamba tulitarajia kuwa mabingwa wa nchi, lakini kutokana na changamoto za hapa na pale matarajio yetu yameshindwa kufanikiwa msimu huu," alisema Jangalu.

Alisema lengo lao kwa msimu wa 2019/2020 lilikuwa ni kuweka historia ya kutwaa ubingwa, lakini kwa kuwa suala hilo limeshindikana, wanajipanga upya kwa ajili ya msimu ujao kwa kuwa inawezekana.

## Kocha Biashara Utd 'jino nje' ligi kurejea

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la Ufundi la Klabu ya Biashara United, limeeleza kuipokea kwa mikono miwili kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli kwa kile alichokisema juzi kuwa anafikiria kuruhusu ligi iendelee.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, alisema kikosi chake kipo tayari kurejea dimbani muda wowote kuendelea na michezo yake iliyobakia.

"Nimeshukuru rais wetu alivyosema anafikiria kuruhusu ligi irudi, ni jambo la msingi kwa sababu wachezaji walikuwa wamekaa tu, japo wanafanya mazoezi ya binafsi," alisema Francis.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wamekuwa makini kufuata maelekezo anayowapa katika kipindi hiki chote cha mapumziko yaliyotokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19).

Wakati akimwapisha, Dk. Mwigulu Nchemba juzi kuwa Waziri wa Katiba na Sheria kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na marehemu Balozi Dk. Augustine Mahiga, aliyefariki dunia Mei Mosi, mwaka huu, Rais Magufuli alisema kwa siku zinazokuja mbeleni anafikiria kuruhusu ligi irejee ili watu angalau wawe wanaangalia kupitia TV na kwamba anachosubiri kwa sasa ni kupata ushauri kutoka kwa wataalamu wake.

Hata hivyo, tayari Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi (TPLB), Almas Kasongo, amesema jana walitarajia kuandaa taarifa kuiomba serikali ligi hiyo irejee rasmi mapema Juni mwaka huu.

# NAMUNGO SASA YAZIONYA SIMBA, YANGA KWA KIKOTI

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Namungo FC ya Lindi, imezionya klabu zinazowanyemelea baadhi ya wachezaji wake, ikidai kuwa wengi wana mikataba mirefu, akiwamo Lucas Kikoti ambaye atabakisha msimu mmoja mwingine baada ya huu kufikia ukingoni.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Zidadu, amesema ni wachezaji wanne tu wa klabu hiyo ambao wanamaliza mikataba yao msimu huu, wakiwamo Reliants Lusajo, Bigirimana Blaise na Nurdin Balora, ambao nao pia wako kwenye mazungumzo ya kuongeza mikataba yao na klabu hiyo.

Mwenyekiti huyo amesema kama kuna klabu inamtaka Kikoti basi iwasiliane na Namungo FC kwa sababu bado ana mkataba, vinginevyo itakuwa inafanya makosa.

**"Najua hawa wachezaji wanahusishwa na klabu mbalimbali kama Simba, Yanga na Azam, lakini Kikoti bado atakuwa amebakisha mkataba wa mwaka mmoja ligi ikiisha kwa sababu tulimsajili kwa mkataba wa misimu miwili, ila tuna wachezaji wanne ambao mikataba yao inamalizika, wakiwamo Lusajo na Bigirimana ambao tunajua wanawindwa na klabu za Simba na Yanga, lakini sisi pia tuko kwenye mazungumzo ya kuwaongeza mikataba," alisema Zidadu.**

Kutokana na hali hiyo, huenda klabu za Simba, Yanga na Azam zikapata wakati mgumu kumsajili winga machachari Kikoti mwenye mabao manne mpaka sasa kwenye msimamo wa Ligi Kuu ambayo imebakisha raundi 10 kabla ya msimu huu kumalizika rasmi.

Hata hivyo, huenda Simba na Yanga zikawa pia na kazi rahisi kuwatwaa Bigirimana na Lusajo.

Timu za Simba na Azam ndizo zinaonekana kumwania zaidi Kikoti, huku Yanga ikiwa inamhitaji zaidi straika Mrundi Bigirimana anayemaliza mkataba, huku akiwa na mabao tisa mpaka sasa.

Simba inatajwa pia kumhitaji straika Lusajo mwenye mabao tisa, ili kuongeza nguvu kwenye kikosi chake, lakini Yanga pia nayo ikinyatia, kama watani zao hao wakizubaa.

**PAMOJA SANA...**



Kipa wa Klabu ya Yanga, Farouk Shikalo (kulia), akiwa na marafiki zake kwao, Mombasa nchini Kenya, baada ya kufanya mazoezi wakati huu klabu yake ikiwa imesitisha mazoezi kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19). **PICHA: MTANDAO**

# *Amri aibadilishia dozi Mbeya City*

**Na Saada Akida**

WAKATI Ligi Kuu Bara ikitarajiwa kurejea mapema Juni mwaka huu, huku timu yake ikiwa katika mstari wa kushuka daraja, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Amri Said amewabadilishia programu ya mazoezi wachezaji wake kwa kuwataka kujifua mara mbili kwa siku kwa ajili ya kujiweka fiti kwa mtifuano huo.

Hadi Ligi Kuu Bara inasimama kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19), Mbeya City ipo nafasi ya nne kutoka mkiani ikiwa na alama 30 baada ya kushuka dimbani mara 29 kwenye ligi hiyo inayojumuisha timu 20.

Kocha huyo ameliambia Nipashe jana, kwamba awali walikuwa wakifanya mazoezi mara moja, ila sasa amewataka wachezaji wake wakiwa nyumbani kujifua asubuhi na jioni.

Alisema amewataka wachezaji wake kutobweteka na mapumziko haya ya corona kutokana na nafasi waliopo.

"Huu si muda wa mchezaji kupumzika, ni kufanya kazi lazima watumie vema muda wa asubuhi na jioni kutumia muda mwingi kwa ajili ya mazoezi ili kuwa fiti," alisema Amri.

Alisema muda huu ni nzuri kuutumia kufanyia kazi mapungufu yao licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu kutokana na wachezaji kuwa mbali naye.

Alisema pia anafanya umuhimu wa kuwajenga kisaikolojia wachezaji wake kwa kutambua thamani ya kipaji chao na wako hapo kwa ajili ya kazi hiyo.

"Huwa nawaambia hii ni kazi ambayo wanatakiwa kupambana kunusuru timu ibaki ili waonekane kwa klabu zingine na kupata nafasi ya kusonga mbele," alisema Amri.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi (TPLB), Almas Kasongo, ligi hiyo inatarajiwa kurejea mapema Juni mwaka huu endapo serikali itaridhia ombi lao walilotarajia kuliwasilisha jana ikiwa ni siku moja baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Dk. John Magufuli kueleza anafikiria kuruhusu ligi hiyo kuendelea baada ya kusimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona.

# Michezo

Jumanne Mei 5, 2020

Nipashe




Dybala, Higuain kubakishwa Juve

UKURASA 22

INAREJEA...




Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia (kulia) na Katibu Mkuu wa shirikisho hilo, Wilfred Kidao, wenye dhamana na soka la Tanzania. **PICHA: MAKTABA**

# Ligi Kuu kurejea Juni

## ●●● TFF, TPLB zafurahia kauli ya Magufuli, masharti makali kutangazwa, vibanda umiza vyatajwa tatizo...

**Na Mwandishi Wetu**

KAULI ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli aliyoitoa Jumapili iliyopita kuwa anafikiria kuruhusu ligi za mpira kuendelea na anachosubiri kwa sasa ni wataalamu wake tu kumshauri, imepokelewa kwa mikono miwili na Shirikisho la Soka nchini (TFF) pamoja na Bodi ya Ligi (TPLB), ambao waliketi juzi jijini Dar es Salaam kujadili hatima ya mtifuano huo.

**Akizungumza na mwandishi wetu jana, Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almas Kasongo, alisema wamepokea kwa furaha kubwa uamuzi wa Rais Magufuli na kwamba wamekubaliana ligi zote kurejea mapema Juni, mwaka huu na kwamba wanachokifanya kwa sasa ni kuandaa taarifa watakayoiwakilisha serikalini ili kupata baraka rasmi.**

Alisema kauli hiyo ya rais imekuja wakati muafaka na iliwakuta wakati wakiwa katika kikao cha kujadili hatima ya ligi hiyo jambo ambalo liliwafanya kutoka na azmio moja la ligi zote kuanzia Ligi Daraja la Pili, la Kwanza na Ligi Kuu kurejea, lakini kwa kuchukua tahadhari zote kama inavyoelekezwa na wizara ya afya.

"Wakati tukiwa kwenye kikao kujadili hatima ya ligi, mara tukasikia kauli hiyo ya rais na baada ya hapo muda wa saa nane tukakubaliana ligi irejee na azimio kuu ni ligi zote, kuanzia Ligi Draja la Pili, la Kwanza na Ligi Kuu zianzie pale zilipoishia kwa staili ile ile ya kucheza nyumbani na ugenini.

"Lakini tulikubaliana ligi itakaporejea tahadhari zote kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuruhusu mashabiki wachche sana na kunawa mikono, hivyo bodi ya ligi na TFF leo asubuhi (jana) tunajipanga kupeleka taarifa serikalini na timu zitapewa nafasi ya kujiandaa," alisema Kasongo.

Kabla ya Rais Magufuli kutoa taarifa hiyo, juzi TFF na TPLB zilikutana kujadili mustakabali wa ligi hiyo kuendelea ama la kutokana na agizo la Shirikisho la Soka Afrika (Caf), kuwataka wanachama wake wote kueleza hatima ya ligi zao kabla ya leo Mei 5, ili kuliwezesha shirikisho hilo kuandaa kalenda zake za michuano mbalimbali.

Lakini akiwa Chato mkoani Geita wakati akimwapisha, Dk. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri wa Katiba na Sheria kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Marehemu Balozi Dk. Augustine Mahiga, aliyefariki dunia Mei Mosi, mwaka huu, Rais Magufuli alisema kwa siku zinazokuja mbeleni anafikiria kuruhusu ligi irejee ili watu angalau wawe wanaangalia kupitia TV.

"Watanzania tusiwe na hofu, tuendelee kuchapa kazi, wanasiasa waache kutumia hii kama ajenda, haitaweza kuwasaidia, Watanzania lazima tuishi, kwa siku zinazoendelea ninafikiri kuruhusu hata ligi za mipira ziendelee, nasubiri wataalamu wangu wanishauri.

"Tuweke utaratibu mzuri kwa sababu ninaelewa hata kwa walioathirika na corona sijaona mwanamichezo mmoja ambaye amedhurika sana kwenye hili na hii inadhihirisha wazi kuwa kwa wale wanaofanya mazoezi corona inawakwepa sasa kama tunawazuia kucheza maana yake tunawaambia waugue corona," alisema Rais Magufuli.

Hata hivyo, wakati Rais Magufuli akitafakari kuhusu kuruhusu ligi hiyo kurejea huku TPLB ikitarajia kuomba irejee mapema Juni, mjadala mkubwa umekuwa ni kwa namna gani mashabiki wataweza kuzingatia masharti kwa kuifuatilia katika TV zao nyumbani na kuachana suala la kwenda katika vibanda umiza kutazama mechi hizo ili kuepuka mikusanyiko.

Ligi zote nchini zilisimama tangu Machi 17, mwaka huu baada ya serikali kupiga marufuku shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo yote kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19) ambavyo vimeua maelfu ya watu duniani.

Hadi jana jumla ya watu 480 nchini waliripotiwa kupata maambukizo ya corona, vifo 16 na waliopona kati ya hao wakiwa 167, na takwimu duniani hadi jana alasiri zinaonyesha jumla ya watu 3,588,267 wamepata maambukizo huku maliopona wakiwa 1,162,712 na vifo vikiwa ni 248,811.

Na hadi ligi hiyo inasimama ikiwa imebakiza takriban raundi 10 kabla ya kumalizika, Simba ilikuwa kileleni mwa msimamo na alama 71, ambazo ni 17 mbele ya Azam FC inayoshika nafasi ya pili, huku Yanga ikiwa ni ya tatu na pointi zake 51, lakini ipo nyuma kwa mchezo mmoja.

# Yanga, Azam zafunguka Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI presha kubwa ya kufutwa kwa Ligi Kuu ilikuwa ikielezwa kuzikumba zaidi Yanga na Azam FC hususan katika nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa, viongozi wa klabu hiyo sasa roho kwatu na wameungana kuipongeza kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Dk. John Magufuli.

Juzi akiwa Chato mkoani Geita wakati akimwapisha, Dk. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri wa Katiba na Sheria kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Marehemu Balozi Dk. Augustine Mahiga, aliyefariki dunia Mei Mosi, mwaka huu, Rais Magufuli alisema kwa siku zinazokuja mbeleni anafikiria kuruhusu ligi irejee ili watu angalau wawe wanaangalia kupitia TV na kwamba anachosubiri kwa sasa ni kupata ushauri kutoka kwa wataalamu wake.

Hata hivyo, jana Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almas Kasongo, alisema wamepokea kwa furaha kubwa uamuzi wa Rais Magufuli na wamekubaliana na TFF ligi zote kurejea mapema Juni, mwaka huu na jana walitarajia kuandaa taarifa watakayoiwakilisha serikalini ili kupata baraka rasmi.

Lakini Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela akizungumza na mwandishi wetu alipongeza kwa kueleza, "Rais Magufuli ni mwanamichezo mwenzetu ametufungulia njia", na kwamba kinachofuata sasa ni kufanya maandalizi kabla ya ligi hiyo kurejea.

Kwa upande wa Ofisa Mtendaji wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema "kauli tumeiona na tumeisikia, tunasubiri wenye mamlaka, litakaloamuliwa lolote tutalipokea, ila tunatambua sisi ni wa pili [kwenye msimamo wa Ligi Kuu]".

Azam FC ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 54 baada ya mechi 28, ikifuatiwa na Yanga yenye pointi 51 zilizotokana na kushuka dimbani mara 28, wakati huu Simba ikiwa kileleni na alama 71, lakini timu zote tatu zimetinga hatua ya robo fainali ya Kombe la FA, linalotoa mwakilishi wa nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >